

MTINDO KATIKA *UTENZI WA KATIRIFU*.

NA

NYAMARI ROSELINE KEMUNTO.

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI
YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

IDARA YA KISWAHILI.

CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

2016

UNGAMO.

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa katika chuo kikuu kingine kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

Nyamari Roseline Kemunto.

Tarehe.

C50/67137/2013.

.....

.....

Kazi hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Prof. Kineene wa Mutiso.

Tarehe.

.....

.....

Prof. Rayya Timammy.

Tarehe.

.....

.....

SHUKRANI.

Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa wafuatao kwa kuchangia kwa njia moja au nyingine ili kuifanikisha kazi hii. Itakuwa vigumu kuwataja wote kwa majina. Shukrani kuu ni kwake Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya, uzima, uwezo na hekima muda huu wote nilipokuwa nikiiandika kazi hii.

Pili, ninawatambua na kutoa shukrani kwa wasimamizi wangu Prof. Kineene wa Mutiso na Prof. Rayya Timammy kwa kunipa mwongozo katika hatua zote nilipokuwa nikiandika kazi hii. Walinifaa katika kuisoma na kuifanyia marekebisha kazi hii hata ikatokea kuwa nzuri na ikakamilika kwa wakati ufaao. Mawaidha waliyonipa yalinifaa katika kuirekebisha na kuiboresha kwa kuiandika upya na vyema kila wakati.

Shukrani nyingine ni kwa wahadhiri wafuatao katika Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Prof. Mwenda Mbatia, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. John Habwe, Prof. Mohamed Abdulaziz, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Nyachae Michira, Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Amiri Swalehe, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Evans Mbuthia na Dkt. Priscah Jerono. Waliniongoza katika kila hatua ya safari hii ya usomi na hata katika kufanya utafiti huu.

Nawashukuru pia wanafunzi wenzangu tulioanza nao safari hii ya usomi. Tulihimizana na kufaana katika kila jambo ndani na nje ya darasa. Nawatakia kila la heri maishani mwao.

Sitamsahau mwanangu Spencer na mpwa Sylvia, ndugu na wazazi wangu Moraa na Nyamari kwa mchango wao katika ulezi wa mwanangu nilipokuwa nikienda shuleni. Sitawasahau marafiki zangu wote.

Mwisho, shukrani ni kwa mwalimu mkuu Bw. Owino Owiso pamoja na walimu wenzangu. Walinisaidia mno kwa kusimamia baadhi ya shughuli zilizohitaji uelekezi wangu nilipokuwa nikifanya utafiti huu. Mola awazidishie katika kila jambo wafanyalo maishani.

IKISIRI.

Utafiti huu umehusu namna ambavyo mtindo umetumika katika *Utenzi wa Katirifu* mswada wa Knappert (1979). Tumehakiki vipengele vya kimtindo ambavyo ni wahusika, taswira, dayalojia na tamathali nyingine za usemi zikiwemo maswali ya balagha, tashihisi, tashibihi, chuku na sitiari. Katika kuhakiki hayo, tumeitumia nadharia ya Umitindo. Tumeongozwa na malengo mawili ya utafiti. Kwanza, kuhakiki vipengele vya kimtindo katika *Utenzi wa Katirifu*na pili, kubainisha umuhimu wa vipengele hivyo katika kuwasilisha dhamira na maudhui ya mtunzi. Kuhusu wahusika, tumehakiki sifa zinazowatambulisha na uhusika wao katika *Utenzi wa Katirifu*. Wahusika wasaidizi wamewasaidia wahusika wakuu katika kujenga na kukamilisha maudhui ya mwandishi. Taswira, dayalojia na tamathali za usemi zimetumiwa kuwasilisha dhamira na maudhui yake. Kuna mandhari ya kijiografia na yale ya kinjozi. Maswali yetu ya utafiti yamepata kujibiwa kikamilifu kwa kuwa tumeweza kubaini vipengele vya kimtindo na pia kuonyesha umuhimu wa vipengele hivyo katika uwasilishaji wa dhamira na maudhui. Hata hivyo, kuna changamoto tulizozipitia. Hatimaye, tumetoa mapendekezo kwa watakaofanya tafiti za baadaye kuhusiana na *Utenzi wa Katirifu*.

YALIYOMO

UNGAMO.....	ii
SHUKRANI	iii
IKISIRI	v
YALIYOMO	vi
SURA YA KWANZA:PENDEKEZO LA UTAFITI.....	1
1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Tatizo La Utafiti	3
1.3 Malengo Ya Utafiti.....	3
1.4Maswali ya Utafiti	3
1.5Sababu za Kuchagua Mada.....	4
1.6 Upeo na Mipaka Ya Utafiti.....	5
1.7 Msingi wa Kinadharia.	5
1.7.1 Kiwango cha maandishi.....	8
1.7.2 Kiwango cha mofolojia.....	9
1.7.3 Kiwango cha kisarufi.....	9
1.7.4 Kiwango cha semantiki.....	10
1.7.5 Mazungumzo na mshikamano.....	10
1.7.6 Muundo na usimulizi.....	10
1.7.7 Itikadi na mtazamo.....	11
1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada.....	12
1.8.1. Yaliyoandikwa kuhusu ushairi.....	12
1.8.2 Yaliyoandikwa kuhusu kazi nyingine za fasihi.....	14
1.9 Mbinu Za Utafiti.....	16
1.10 Hitimisho.....	17

SURA YA PILI:WAHUSIKA NA UHUSIKA WAO KATIKA UTENZI WA KATIRIFU.....	18
2.1 Utangulizi	18
2.2 Uhusika na wahusika.....	18
2.3 Mbinu za kuwasawiri wahusika.....	19
2.3.1 Matendo au matumizi ya mazungumzo.....	20
2.3.2 Maelezo au masimulizi yanayotolewa na mtunzi / mwandishi.....	21
2.3.3 Maelezo kutokana na wahusika wengine.....	21
2.3.4 Matumizi ya majina ya kimajazi na lakabu.	21
2.3.5 Mbinu ya mgotanisho.....	22
2.4 Umakundi wa wahusika.....	22
2.4.1 Wahusika wakuu.....	23
2.4.1.1 Katirifu.....	23
2.4.1.2 Hasina.....	26
2.4.1.3 Mtume Muhammad. (S.A.W).....	29
2.4.2 Wahusika wasaidizi.....	31
2.4.2.1 Amri.....	31
2.4.2.2 Mchungaji.....	33
2.4.2.3 Ali.....	33
2.4.2.4 Babake Hasina.....	36
2.4.2.5 Kidari.....	36
2.5 Hitimisho.....	37
SURA YA TATU:TASWIRA, DAYALOJIA NA TAMATHALI ZA USEMI. ..	38
3.1 Utangulizi.....	38
3.2 Taswira.....	39
3.3 Dayalojia.....	40
3.4 Tamathali za usemi.....	41
3.4.1 Maswali ya balagha.....	42

3.4.2. Tashihisi / Uhuishaji.	44
3.4.3 Tashibihi.	45
3.4.4 Chuku.	48
3.4.5 Sitiari.	50
3.5 Uhuru wa Kishairi.	51
3.5.1 Inkisari.	51
3.6 Lahaja.	52
3.7 Matumizi ya Kiswahili cha kale au zamani.	52
3.8 Hitimisho.	53
SURA YA NNE:MANDHARI NA USIMULIZI.	54
4.1 Utangulizi.	54
4.2 Mandhari.	55
4.2.1 Mandhari halisi.	55
4.2.2 Mandhari ya kinjozi.	59
4.3 Usimulizi.	60
4.3.2 Mbinu za usimulizi.	61
4.3.2.1 Usimulizi wa nafsi ya kwanza.	62
4.3.2.2 Usimulizi ngazi.	63
4.3.2.3 Usimulizi wa nafsi ya tatu.	65
SURA YA TANO:HITIMISHO.	70
5.1 Muhtasari wa Yaliyoshughulikiwa Katika Utafiti Huu.	70
5.2 Changamoto.	71
5.3 Mapendekezo kwa Tafiti Za Baadaye.	71
MAREJELEO.	73

SURA YA KWANZA

PENDEKEZO LA UTAFITI

1.1 Utangulizi.

Abedi (1954) anasema kuwa utenzi ni ushairi wenye mizani chache kuliko kumi na mbili, ambao mara nyingi hauna vina vya kati katika mistari, bali kila ubeti una vina vya namna moja katika mistari yake isipokuwa mistari wa mwisho katika kila ubeti, ambao huendelea na kina cha namna moja kinachoitwa bahari.

Tenzi nyingi hugawika katika mishororo minne. Idadi ya mizani hutofautiana kutoka utenzi mmoja hadi mwingine. Ingawa kila mtunzi wa utenzi huchukua muundo mmoja katika uwasilishaji, maudhui na dhamira za kazi zenyewe hutofautiana. Aghalabu tenzi nyingi husimulia kuhusu dini, maadili, malezi na utamaduni. Mtunzi wa *Utenzi wa Katirifu* ameegemea mno upande wa dini na maadili kimaudhui.

Utenzi wa Katirifu ni utenzi wa kidini. Ni kati ya tenzi za kale zaidi kwa kuwa lugha iliyotumika na tarehe ulipoandikwa ni ya zamani. Ulitungwa baada ya *Hamziya* na *Utenzi wa Herekali*. Mtunzi ni Bakari Mwengo. Ni mwanawe mtunzi wa *Utenzi wa Herekali* au *Utenzi wa Tambuka* zilizotungwa na Mwengo Athmani.

Utenzi huu umepewa anwani *Utenzi wa Katirifu* kwa kuwa mhusika mkuu ni Katirifu. Wahusika wengine ni Amri, Hasina, Mchungaji, Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali. Babake Hasina aliuliwa katika vita vya Badri-vita kati ya Waislamu na makafiri. Mtume Muhammad (S.A.W) alishiriki vita hivyo kwa kuwa hakupenda maovu na hivyo Hasina anataka kulipiza kisasi. Katirifu anauliwa vitani.

Mtunzi ametoka Pate lakini ametumia lahaja ya Kiamu kwa kuwa ndiyo lahaja iliyotumika wakati huo. Utenzi huu pia huitwa *Utenzi wa Wadi Isbani* au *Utenzi wa Ghazwa Sesebani*. Mswada tuliutumia kuhakiki mtindo ni ule wa Knappert (1979).

Utafiti huu unahusu namna ambavyo mtindo umetumika katika *Utenzi wa Katirifu*. Senkoro (1982) anaufafanua mtindo katika fasihi kuwa namna ambavyo msanii hutunga kazi na kuipa sura ambayo kifani na kimaudhui huainisha kanuni zilizofuatwa za kimapokeo. Fani na maudhui hupangwa ili kuonyesha upekee wa mtunzi husika. Kazi ya mtunzi huweza kuangaliwa kwa namna alivyoipanga. Uwasilishaji wa jambo moja kupitia watunzi wawili huweza kutofautiana. Kunakuwa na upekee katika uwasilishaji.

Wamitila (2002) anasema kuwa mtindo ni jumla ya mbinu anazozitumia mtunzi katika kutunga kazi ya fasihi. Ni sifa maalum za mwandishi. Ni mbinu za kijumla za uandishi wa kazi husika kama vile uteuzi wa msamiati, aina ya sentensi, uakifishi na tamathali za usemi. Wataalam hawa wawili wametilia msisitizo kwenye upekee katika uwasilishaji. Njogu na Chimera (1999:384) wanasema kuwa mtindo ni mseto wa fani na maudhui.

Katika utafiti wetu, tumehakiki vipengele vya kimtindo vinavyojitokeza katika *Utenzi wa Katirifu* uliotungwa na Mwengo Athmani. Tumeonyesha uhusiano uliopo kati ya vipengele vya kimtindo katika kufanikisha dhamira ya mtunzi huyu. Tumeichagua nadharia ya Umitindo ili itufae katika kuhakiki vipengele vya kimtindo vilivyotumika katika *Utenzi wa Katirifu*.

1.2 Tatizo La Utafiti.

Katika utafiti huu tumebainisha namna mtunzi wa *Utenzi wa Katirifu* anavyotumia vipengele vya kimtindo hasa wahusika na uhusika wao, matumizi ya lugha, mandhari, ploti na usimulizi katika kuifanikisha dhamira ya mwandishi.

Fani na maudhui haviwezi kutenganishwa ila huangaliwa kwa pamoja kwa kuwa vinaingiliana na kukamilishana. Watafiti wengi katika tafiti zao wameegemea mno kuangalia vipengele hivi katika upande wa tamthilia na riwaya. Kanyua (2011) ameshughulikia mtindo na namna unavyoendeleza maudhui katika tamthilia ya *Natala*. Murumba (2011) amefanya uhakiki wa mtindo katika riwaya ya *Watu wa Gehena*. Hata hivyo kuna baadhi ya watafiti walioshughulikia ushairi. Lugwiri (2011) ameshughulikia vipengele vya kimtindo-sitiari, taashira na tashibiha na mchango wao katika uwasilishaji wa dhamira katika *Utenzi wa Tambuka*.

Utafiti wetu umeonyesha kuwa vipengele vya kimtindo katika ushairi na hasa tenzi za Kiswahili pia haviwezi kushughulikiwa katika upekee ila vinachangiana na kukamilishana namna ilivyo katika tanzu nyingine za fasihi. Tumetumia *Utenzi wa Katirifu* katika kubainisha hayo.

1.3 Malengo Ya Utafiti.

- i) Kuhakiki vipengele mbalimbali vya kimtindo vilivyotumika katika katika *Utenzi wa Katirifu*.
- ii) Kubainisha umuhimu wa vipengele vya kimtindo katika kuwasilisha dhamira na maudhui ya mwandishi katika *Utenzi wa Katirifu*.

1.4 Maswali ya Utafiti.

- i) Je, vipengele mbalimbali vya kimtindo vimetumiwa vipi katika *Utenzi wa Katirifu*?

ii) Je, matumizi ya vipengele mbalimbali vya kimtindo yamesababisha uwasilishaji mwafaka wa dhamira na maudhui katika *Utenzi wa Katirifu*?

1.5 Sababu za Kuchagua Mada.

Watafiti wengi hawajaegemea upande wa kuchanganua vipengele vya kimtindo katika tenzi. Vipengele vingi vilivyofanyiwa utafiti vimejikita mno katika tanzu nyingine za fasihi kama vile tamthilia, riwaya na hadithi fupi. Baadhi ya tenzi zilizoshughulikiwa ni *Utenzi wa Tambuka*, *Utenzi wa Mwanafatuma* na *Utenzi wa Adamu na Hawa*. Utafiti huu umeonyesha kuwa mtindo pia hupatikana na kutumika katika tenzi na wala si katika riwaya, tamthilia na hadithi fupi tu. Hivyo, tenzi hazifai kudunishwa.

Katika tenzi nyingi zilizotafitiwa, watafiti wameegemea mno uchanganuzi wa maudhui. Tumelenga kuonyesha namna vipengele vya kimtindo vinatumika katika kukamilisha dhamira ya mwandishi. Katika kazi yoyote ile ya fasihi, vipengele vya kimtindo huchangiana na kukamilishana ili kufanikisha dhamira ya mtunzi. Tenzi zikiwa mojawapo ya kazi hizo za fasihi.

Kutokana na tasnifu mbalimbali tulizopitia zinazoshughulikia tenzi, hakuna unaofanana moja kwa moja na ule tumeufanya kuhusu mtindo katika *Utenzi wa Katirifu*. Utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa wahakiki wa baadaye katika kuhakiki mtindo katika tenzi nyingine za Kiswahili. Utafiti huu utakuwa kama msingi kwa watafiti walio na lengo la kuhakiki mtindo katika tenzi nyingine. Mtindo uliotumika katika utenzi huu huenda ukawa tofauti ule uliotumika katika tenzi nyingine.

Tumeuchagua *Utenzi wa Katirifu* kwa kuwa hatujapata ushahidi wowote kuwa utenzi huu umeandikiwa. Makala na tasnifu nyingi hazijaandikwa kuhusu *Utenzi wa Katirifu*. Msukumo wetu wa kuandika kuhusu kazi hii ulitokana na mafunzo ya

darasani ambapo utenzi huu ulikuwa miongoni mwa kazi teule tulizozishughulikia. Watafiti wengi hawapendi ushairi kwa hivyo hii itakuwa njia ya kuwafanya kuupenda.

1.6 Upeo na Mipaka Ya Utafiti.

Katika utafiti wetu, tumejikita kwenye vipengele vya kimtindo na namna ambavyo vimekuza dhamira ya mtunzi wa *Utenzi wa Katirifu*. Tumeshughulikia vipengele vya kimtindo kama vile wahusika, tamathali za usemi, usimulizi na mandhari katika *Utenzi wa Katirifu* na mchango wake katika kukuza na kuendeleza dhamira ya mwandishi. Kuhusu wahusika tumeangalia sifa zao, mbinu zilizotumiwa kuwasawiri na mchango wao katika kukuza na kuendeleza dhamira ya mwandishi huyu.

Taswira, dayalojia na tamathali za usemi kama vile maswali ya balagha, tashihisi, tashibihi, chuku na sitiari zimetumia ukiushi wa kisemantiki ili kuwasilisha ujumbe. Mandhari na usimulizi pia vimesaidia kurahisisha kueleweka kwa utenzi wenyewe. Kuna tenzi na kazi nyingine kama vile riwaya na tamthilia zinazoweza kuhakikiwa kwa kutumia nadharia ya umitindo. Hata hivyo, tumerejelea kazi nyingine zinazohusiana na hii na kupata mchango ulioweza kuikamilisha.

1.7 Msingi wa Kinadharia.

Nadharia tunayoitumia katika kuhakiki mtindo wa kazi hii ni moja. Tumeichagua nadharia ya Umitindo. Sababu ya kuichagua nadharia hii ni kuwa tumehakiki mtindo katika *Utenzi wa Katirifu* na katika mtindo kuna kipengele cha tamathali za usemi. Katika utafiti wetu kwa kiwango kikubwa tumejikita katika vipengele vifuatavyo vya kimtindo: wahusika, matumizi ya lugha, mandhari, ploti na usimulizi. Tumeangazia namna vipengele hivyo vimetumika na mtunzi wa *Utenzi wa Katirifu*. Jambo hili linatufanya kujikita katika nadharia ya Umitindo.

Nadharia ya Umitindo ina misingi yake Urusi. Iliasisiwa mwaka 1904. Mbatia (2001) anasema kuwa nadharia hii iliibuka Moscow mwanzoni mwa karne ya 20 na iliasisiwa kwa nia ya kuelezea kuwa fasihi ni matumizi ya pekee ya lugha, tofauti na lugha ya kawaida. Fasihi ilifaa kumwezesha msomaji au msikilizaji kuona kitu upya. Viktor Shyklovsky na Mbatia wana mwelekeo unaofanana kwa kuwa wanaona kuwa sanaa hufanya kitu kuonekana kipya hivyo fasiri mpya kuhusu kitu hicho kutolewa.

Nadharia hii inaonyesha umuhimu wa lugha katika kuelezea maana ya fasihi. Ililenga kuainisha sifa za kisanaa katika fasihi kama taaluma. Mwasisi ni Viktor Shklovsky aliyelandika kuhusu 'ufufuo wa neno' alikozungumzia umuhimu wa lugha katika kuelewa maana ya fasihi.

Waasisi wa Umitindo walielekea kugegemea mno upande wa ushairi kwa kuwa mashairi yalikuwa kazi za awali kabisa kuandikwa na yalikuwa mepesi katika uwasilishaji wake. Yangewasilishiwa popote kama vile njiani, jukwaani, kanisani, mikahawani na hata mikutanoni. Sheria zilizohusiana na ushairi kama vile vina, mizani na sauti zilitiliwa maanani. Uhuru wa mshairi na namna ya kutunga viliangaliwa kwa makini.

Kulingana na Wamitila (2003) anasema kuwa kilichokuwa muhimu ni fasihi yenyewe. Ushairi ulikuwa muhimu kuliko mshairi mwenyewe. Lugha iliyotumiwa ilitegemea mno utanzu wa fasihi uliohusika. Fasihi ilichunguzwa kisayansi ili kubaini kazi inayotekelezwa na lugha katika fasihi. Kazi zote zilifanyiwa uchunguzi kisayansi. Sifa zilizotambulisha fasihi zilibainishwa. Kazi za watu binafsi ziliangaliwa ili kubainisha ufasihi wao. Kwa kifupi, nadharia hii inatilia mkazo lugha ilivyotumika katika kazi na wala si mwandishi katika uwasilishaji wa kazi ya fasihi.

Leech (1969) anaelezea kuwa mtindo ulihusishwa na isimu. Isimu hujihusisha na usomaji na ujifunzaji wa lugha hasa lugha ya kifasihi. Katika kipindi hicho mitazamo miwili ilitokea-uile wa kiisimu na mwingine wa kifasihi. Hata hivyo, ilibainika kuwa isimu na fasihi yalikuwa mambo mawili tofauti ambayo hayakuwa na uhusiano wowote.

Leech anaelezea elimumitindo kuwa uwanja unaojishughulisha na maswala ya kiisimu na vilevile ya kifasihi. Mambo haya hayawezi kuchanganuliwa katika upekee wake ila yanachangiana na kukamilishana. Ni ile hali ya kuchunguza lugha ilivyotumika katika uwanja mwingine.

Nadharia hii ina sifa kama vile kuwepo kwa kanuni zinazosaidia katika kuwateua wahusika kulingana na lugha inayotumiwa. Hivyo, lugha tumizi inamtambulisha mhusika fulani. Pili, kuna matumizi ya mazungumzo ama dayalojia katika kazi husika na sarufi kwa jumla na matumizi ya sauti na urefu katika sentensi zilizotumika.

Athari inayotokana na kazi iliyoandikwa inatokana na mtindo uliotumika na jambo hili si katika kazi za kifasihi tu bali pia katika mazungumzo. Umitindo basi ni namna ya kuchanganua mtindo kisayansi hasa katika kazi za kifasihi. Ushairi ukiwa mojawapo kati ya tanzu za fasihi.

Wamitila (2003) anasema kuwa Umitindo unaweza kutumiwa katika uhakiki wa kazi za fasihi pamoja na zile za kiisimu. Katika uhakiki huo si lugha tu inayochunguzwa bali vipengele vyote vya kifani na vilevile kimaudhui huchunguzwa. Maoni haya yanashabihiana na yale ya Leech (1981).

Ufasihi ulipewa kipaumbele katika fasihi. Lugha ya kishairi ilitambuliwa kutokana na matumizi ya maneno kisanaa. Msomaji hupata maana ya fasihi iliyoundwa kwa kuangalia miundo ya matini zenyewe. Mwandishi huondolewa katika kazi yake na mambo yanayomhusu kama vile historia yake. Fasihi huwa na muundo uliokamilika vipengele vinapowekwa pamoja. Tamathali za usemi ni baadhi ya vipengele vinavyotumika katika fasihi.

Crystal na Davy (1969) katika mtazamo wao wanasema kuwa lengo kuu la Umitindo ni kuziweka wazi sifa mahsusi zinazopatikana katika muktadha fulani. Mbatia (2001) anatilia mkazo kauli hii ya ufasihi kwa kusema kuwa ufasihi wa fasihi ni matumizi ya kipekee ya lugha. Ufasihi hutofautisha fasihi na sanaa nyingine. Ufasihi katika *Utenzi wa Katirifu* ndio unaotupelekea katika kuchunguza tamathali za lugha. Tumeangalia ukiushi ulivyotumika ili kuibua ufasihi kupitia tamathali za usemi.

Kabla ya kufanya uhakiki wa mtindo katika fasihi yoyote ile, kuna viwango mbalimbali vya ukiushi vinavyoangaziwa navyo ni: ukiushi wa kimsamiati, ukiushi wa kisarufi, ukiushi wa kilahaja, ukiushi wa sajili au rejesta, ukiushi wa kifonolojia, ukiushi wa kimaandishi, ukiushi wa kihistoria na ukiushi wa kisemantiki.

Hata hivyo, Wamitila (2008) anasisitizia mambo yafuatayo kuwa muhimu zaidi katika uhakiki wa mtindo katika fasihi. Anazungumzia lugha ya kitamathali, uteuzi wa mtindo, usimulizi, mtazamo na itikadi, muwala, mshikamano na mazungumzo.

Mambo muhimu yanayojitokeza katika viwango tofauti ni kama ifuatavyo:

1.7.1 Kiwango cha maandishi.

Maandishi hutokea kwa namna mbili-namna lugha inavyotamkwa au vile ambavyo lugha hiyo inaandikwa. Hiyo inajikita katika viwango vya fonetiki na fonolojia katika

isimu. Katika kiwango hiki maneno yanaweza kubadilishwa kimatamshi au kimaandishi. Kwa mfano, neno mwizi linaweza kuwa mwivi. Alama za uakifishi pia huweza kutumika kuleta maana fulani iliyokusudiwa na mwandishi. Kwa mfano, matumizi ya herufi kubwa katika neno lote, alama za kuonyesha hisi ili kuonyesha hisia za mhusika fulani, koloni, vistari au hata zile za kuulizia maswali.

1.7.2 Kiwango cha mofolojia.

Kwa kawaida lugha tumizi ndiyo inayotumika kuwasilisha ujumbe. Katika kiwango cha umbo maneno mapya huweza kuundwa kutokana na maneno yaliyopo. Kwa mfano kitenzi kinaweza kuundwa kutokana na nomino. Kwa mfano, nomino wimbo inaweza kuunda kitenzi imbika. Maneno kama haya yanapoundwa kwa kiwango kikubwa hayafuati kanuni za kisarufi za lugha inayohusika. Katika uandishi utapata matumizi ya maneno ya kilahaja, kutumia msamiati uliochukuliwa kutoka lugha nyingine, kuhamisha ndimi na utohozi wa maneno pia unaweza kufanywa. Uundaji huu upya wa maneno ukitokea utaonyesha mabadiliko katika maumbo ya maneno. Maneno ya kizamani pia hutumiwa kwa mfano, ngeu linatumika kumaanisha damu na insi kurejelea binadamu.

1.7.3 Kiwango cha kisarufi.

Sarufi ndio msingi wa lugha yoyote ile. Katika kiwango hiki, lugha ya kimatamshi au kimaandishi hudhibitiwa na sheria za kiisimu. Mofolojia na sintaksia huzingatiwa katika kiwango hiki. Mpangilio utajikita kwenye mofolojia ilhali sentensi zinakuwa katika kiwango cha sintaksia-ule mpangilio wa maneno ili kuunda sentensi. Matumizi ya takriri yaani kurudia silabi, maneno au vifungu vya maneno. Kurudia neno moja katika sentensi huweza kuwa katika kiwango hiki. Lahaja mbalimbali kutumika katika kazi ya fasihi husika hivyo kuibua sentensi tofauti kimatamshi lakini maana huwa ni moja.

1.7.4 Kiwango cha semantiki.

Hiki ni kiwango kinachojihusisha na maana. Ni kiwango kinachoshughulikia maana iliyoibuka kutokana na msamiati uliotumika. Namna ambavyo msikilizaji au msomaji atakavyofasiri huathiri kwa kiwango kikubwa maana ya kawaida. Maana ya neno hufasiriwa kwa njia mbalimbali. Ni kana kwamba katika usemi kuna maana ya nje na ile ya ndani. Tamathali za usemi huhakikiwa katika kiwango hiki. Tamathali kama vile kweli-kinzani, kinaya, kejeli, sitiari na jazanda hutumika. Tamathali hizi huwa na maana wazi pamoja na fiche. Msomaji au msikilizaji hufasiri maneno kwa njia tofauti.

1.7.5 Mazungumzo na mshikamano.

Wahusika wanapowasiliana kwa mazungumzo wanayatumia kama mbinu ya kuwasilisha mawazo yao. Ujumbe muhimu unaweza kupitishwa kupitia kwa mazungumzo hayo. Wamitila (2008) anasema kuwa mazungumzo baina ya wahusika na mbinu nyingine hutumika katika mazungumzo kwa nia ya kubainisha mawazo yaliyokusudiwa na mwandishi husika. Mambo fulani kama vile elimu huweza kumtambulisha mhusika. Lugha ya kwanza hutumiwa na watu ambao hawajasoma ilhali Kiswahili na Kiingereza kutumiwa na wale waliosoma.

1.7.6 Muundo na usimulizi.

Muundo unamaanisha namna kazi yenyewe ilivyopangwa. Msuko utafafanua namna matukio ya kazi yalivyopangwa. Hii huifanya kazi husika kuwa tofauti na kazi nyingine zinazoelekea kuwa na maudhui sawa na ile inayozungumziwa. Matukio katika kazi ya fasihi huendana na wakati. Mbinu rejeshi hutumika tu pale ambapo mwandishi anaturejesha kutuelezea kuhusu matukio yaliyowahi kutendeka hapo awali ambayo hayakupata kusimuliwa pale mwanzoni.

Usimulizi unaohusiana na kutoa maelezo unaweza kutumika katika kufafanua au kuelezea jambo fulani. Ni mpangilio wa uwasilishaji wa matukio na msuko. Matukio katika kazi yoyote ya fasihi hufuata mpangilio fulani. Masimulizi yanaweza kuwa ya moja kwa moja au yasiwe.

Kuna mhusika anayesimulia matukio katika fasihi hivyo kuifanya nafsi pia kubadilika kutoka kazi moja hadi nyingine. Kazi inaweza kuwa na matumizi ya nafsi ya kwanza, pili au tatu. Mhusika pia anaweza kubadilishwa na mwandishi kutoka nafsi moja hadi nyingine.

Muundo wa kazi ya fasihi huwa na mwanzo, kati na mwisho. Mwanzo huwa ni utangulizi wa kisa au mkasa fulani, kati huwa na mgogoro ambao aghalabu unahusisha pande mbili na mwisho ambao huwa ni suluhisho la mgogoro uliokuwa umetangulizwa pale mwanzoni. Ikiwa mgogoro huo hautatatuliwa, kazi husika huishia katika taharuki.

1.7.7 Itikadi na mtazamo.

Kila mwandishi huchukua itikadi na mtazamo tofauti. Anachukua mkabala fulani katika kuelezea maswala yake yote. Wamitila (2008) anasema kuwa kutokana na mtazamo wa mwandishi basi mhakiki anaweza kuchanganua mwelekeo na msimamo wa kimawazo wa mwandishi. Uteuzi wa msamiati huangaliwa katika kiwango hiki.

Hatujavitumia viwango hivi vyote ila tumeteua vile ambavyo vimeafiki utafiti wetu ambavyo ni: kiwango cha muundo na usimulizi, mofolojia, semantiki na sarufi. Katika muundo na usimulizi tumeangalia matumizi ya mbinu rejeshi katika kuwasilisha matukio ya utenzi huu. Sitiari, taswira na tashibihi hujikita katika kiwango cha semantiki ilhali takriri, kuhamisha ndimi, utohozi na matumizi ya maneno ya kale vimehakikiwa katika kiwango cha mofolojia.

1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada.

Mapitio yetu kuhusu yaliyoandikwa kuhusu mada yetu yamejikita kwenye mashairi ya Kiswahili hasa yale ya kale-yaliyoandikwa kabla ya karne ya ishirini. Hii ni kwa kuwa tenzi nyingi ziliandikwa wakati huo. Suala la mtindo limeshughulikiwa mno katika tanzu nyingine za fasihi kama vile riwaya na tamthilia na wala si katika tenzi. Hata hivyo, kuna baadhi ya tafiti kuhusu tenzi kama vile: *Utenzi wa Tambuka*, *Utenzi wa Adamu na Hawa*, *Utenzi wa MwanaFatuma* na nyingine nyingi. Hii imetupa nafasi ya kutafitia mtindo katika utenzi huu.

Hakuna utafiti uliofanywa unaofanana moja kwa moja na ule ambao tumeufanya kwani kila utafiti umechukua mkabala tofauti na ule tumeuchukua. Tafiti nyingi zilizofanywa ni kuhusu mtindo unavyowasilisha dhamira ya mwandishi katika utanzu wa riwaya na vilevile tamthilia. Katika sehemu hii tumezigawa kazi tulizozirejelea katika makundi mawili: kwanza zile zinazohusu utanzu wa ushairi kisha zile zilizotafiti tanzu nyingine hasa riwaya na tamthilia.

1.8.1. Yaliyoandikwa kuhusu ushairi.

Kadenge (1982) katika tasnifu yake anaelezea kuhusu dhana za ukiushi na uchimuzi. Anazifafanua kuwa ni hali ya kukiuka sheria zinazotawala matumizi ya lugha. Ni ukiushi wa kimakusudi wa lugha kwa madhumuni ya kusisitiza ujumbe katika kazi fulani ya kifasihi. Katika tasnifu yake, anaonyesha kuwa vipengele vya ukiushi huchukua jukumu la mawasiliano na hivyo kuchukuliwa kuwa mwandishi huvitumia ili kupitisha ujumbe kwa msomaji. Ameshughulikia kazi tatu: riwaya ya *Asali Chungu*, tamthilia ya *Wakati Ukuta* na utenzi wa *Swifa ya Nguvumali*. Kulingana na kazi yake, umitindo unachukuliwa kuwa daraja kati ya muundo na yanayoshughulikiwa katika kazi ya fasihi. Si kazi yake nzima imetufaa. Tumejiikita katika sura ya pili alikoandika kuhusu matumizi ya mtindo katika utenzi wa *Swifa ya*

Nguvumali. Uhakiki alioufanya umetufaa kwa kuwaamehakiki ukiushi ambao pia tumeuhakiki kwa kuwa tumejikita katika ushairi. Tofauti iliyopo ni kuwa tumehakiki mtindo katika kazi moja tu ambayo ni *Utenzi wa Katirifu*.

Kitsao (1975) katika tasnifu yake amehakiki namna mtindo ulivyotumiwa katika kazi mbalimbali za fasihi. Ameangazia tamthilia, riwaya na mashairi teule katika kufanya utafiti wake. Katika tasnifu yake ameonyesha mtindo na elimumtindo zinavyotumika katika kazi mbalimbali za kifasihi. Pia, ameutumia mtazamo wa Crystal na Davy (1969) uliohusu lugha inayotumika. Utafiti wa Kitsao umetufaa kwa kuwa umetupa mwelekeo katika utafiti wetu kwa vile tumeangalia mtindo katika ushairi tukijikita katika *Utenzi wa Katirifu*. Nadharia tuliyoichagua ni ile ya Umitindo aliyoitumia Kitsao katika kuhakiki mtindo. Mkabala tuliouchukua ni tofauti kwa kuwa tumejikita katika kazi moja ambayo ni utenzi na tumehakiki vipengele mahsusi vya kimtindo.

Lugwiri (2011) ameshughulikia vipengele vya kimtindo ambavyo ni sitiari, taashira na tashibiha na mchango wa vipengele hivyo katika uwasilishaji wa dhamira na maudhui katika *Utenzi wa Tambuka*. Lugwiri ametumia nadharia ya Umitindo katika kuhakiki vipengele hivyo. Ameonyesha kuwa tamathali za lugha huchangia pakubwa katika kukuza na kuendeleza maudhui na dhamira. Utafiti huu umetufaa kwa kuwa tumehakiki pia vipengele vya kimtindo katika *Utenzi wa Katirifu* na nadharia tuliyoichagua katika uhakiki wa mtindo katika utafiti wetu ni ile ya Umitindo. Tofauti ni kuwa Lugwiri amehakiki *Utenzi wa Tambuka* ilhali tumehakiki *Utenzi wa Katirifu*.

Ouma (2011) ameshughulikia uhakiki wa maudhui teule katika *Utenzi wa NabiiIsa*. Ameitumia nadharia ya Uyakiniifu wa kijamii katika kuyahakiki maudhui hayo. Kazi yake itatufaa kwa kuwa ameshughulikia utenzi kama tulivyoshughulikia na maswala

yanayozungumziwa katika tenzi hushabihiana. Tofauti ni nadharia aliyoitumia ambayo ni Uyakunifu wa kijamii nasi tumeitumia nadharia ya Umitindo .

1.8.2 Yaliyoandikwa kuhusu kazi nyingine za fasihi.

Murumba (2011) amefanya uhakiki wa mtindo katika riwaya *Watu wa Gehena*. Katika utafiti wake ameonyesha viwango vyote vya mtindo na namna unavyohakikiwa na hivyo kazi yake imekuwa ya manufaa makubwa mno kwetu kwa kuwa tumehakiki mtindo katika ushairi. Tumeitumia kazi yake kama kielelezo tu katika kufanya utafiti wetu. Tofauti kati ya utafiti wake na wetu ni kuwa ameshughulikia riwaya ilhali sisi tumeshughulikia utenzi .

Kanyua (2011) ameshughulikia mtindo na namna unavyoendeleza maudhui katika tamthilia ya *Natala*. Nadharia alizozitumia ni ile ya Umuundo na Ufeministi wa Kiafrika. Ametumia umuundo katika kuchanganua vipengele vya kimtindo na Ufeministi katika kuhakiki maudhui. Utafiti wake umenifaa kwa kuwa katika kazi yake amechanganua vipengele vya kifani kama vile matumizi ya lugha na wahusika ambavyo pia tumeviangazia katika utenzi tuliouteua. Tofauti ni kuwa katika uhakiki wake amejikita kwenye tamthilia ya *Natala* nasi tumejika katika *Utenzi wa Katirifu*. Pili, ametumia nadharia za Umuundo na Ufeministi wa Kiafrika ilhali sisi tumetumia nadharia ya Umitindo.

Nzuki (2003) katika utafiti wake ameshughulikia mwingiliano wa vipengele vya fani na maudhui. Amejikita katika diwani mbili ambazo ni *Mchezo wa Karata (1997)* na *Bara Jingine (2001)*. Ametumia nadharia mbili. Ametumia Umuundo na Nadharia ya Kisoshiolojia katika kufanya utafiti wake. Ameonyesha namna ambavyo vipengele vya kimtindo huchangiana ili kukamilisha kazi nzima ya fasihi. Utafiti wa Nzuki unakaribiana mno na utafiti tumeufanya. Utafiti wa Nzuki umetupa mwongozo

uliotusaidia katika utafiti wetu. Aliyoyashughulikia ambayo ni mwingiliano wa vipengele vya kimtindo na maudhui na jukumu la vipengele hivyo katika kukamilisha dhamira ya mwandishi. Utafiti wake umekuwa nguzo kuu katika kufanya utafiti wetu. Tofauti ni kuwa ametumia nadharia za Umuundo na Kisoshiolojia ilhali katika utafiti wetu tumetumia nadharia za Umitindo katika kuhakiki vipengele vya kimtindo. Pili, amehakiki diwani mbili: *Mchezo wa Karata* (1997) na *Bara Jingine* (2001) ilhali tumejikita katika utenzi mmoja tu- *Utenzi wa Katirifu* tuliouteua kutoka katika baadhi ya matini tulizozipitia darasani.

Swaleh (1992) amehakiki maudhui katika *Utenzi wa Mwanakupona*. Anazungumzia namna dini inavyomwathiri mwanamke hasa mwanamke wa Kiislamu. Majukumu aliyopewa mwanamke yanaelekea kumdhulumu. Tumeonyesha mtindo na mchango wake katika kukuza maudhui. Ameshughulikia maudhui katika kazi yake nasi tumehakiki kipengele kimoja tu ambacho ni mtindo. Kazi tulizozishughulikia ni tofauti kwa kuwa Swaleh amehakiki *Utenzi wa Mwanakupona* nasi tukahakiki *Utenzi wa Katirifu*.

Muthoni (2014) amehakiki maudhui na mtindo katika riwaya *Tikitimaji*. Ametumia nadharia ya Umitindo katika kuhakiki mtindo na uhalisia katika kuhakiki maudhui yanayojitokeza katika riwaya hiyo. Utafiti huu umenifaa zaidi kwa kuwa tumeshughulikia mtindo. Hata hivyo, kazi ya fasihi tuliyoiteua ni tofauti kwa kuwa ni ushairi naye ameshughulikia riwaya. Imefanana tu katika upande wa matumizi ya nadharia ambapo kazi zote zimetumia nadharia ya Umitindo.

Mungai (2005) ameangazia fani katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*. Vipengele vya fani vilivyochanganuliwa katika utenzi vimeshabihiana na vile tumehakiki katika utafiti wetu ila tenzi tulizoziteua ni tofauti.

1.9 Mbinu Za Utafiti.

Mwanzo, tumeisoma kazi teule kwa kina tukijikita katika kuangazia matumizi ya vipengele vya kimtindo katika kuwasilisha dhamira ya mwandishi. Tumesoma tenzi nyingine za Kiswahili hasa zile zilizoandikwa kabla ya karne ya ishirini. Tenzi nyingi zilizoandikwa wakati huo zinakaribiana mno katika uwasilishaji na maudhui yanayozungumziwa. Tumefanya utafiti wa kina kamaelezo wala si kitakwimu kwa kuwa mada tunayoishughulikia inahusu mno usomaji wa vitabu na makala yaliyoandikwa kuhusu tenzi na vitabu hivyo ili kupata uelewa wa kina zaidi kuhusu mada ambayo tumeishughulikia.

Tumezisoma kazi nyingine zilizofanywa na watafiti wengine hasa waliogusia mtindo. Pia, tumeangalia maandishi yaliyoandikwa na wataalamu mbalimbali kuhusu nadharia ya Umitindo. Tumezipitia kazi za wasomi wengine kuhusu mtindo katika riwaya na tamthilia lakini zaidi tukijikita katika mtindo uliotumika katika kazi za Kiswahili ili tupate maarifa zaidi kuhusu uwanja wetu wa utafiti. Tumeutumia mtandao katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu ya kuwa mengi yameandikwa kuhusu tenzi na kuwekwa katika mtandao. Tafiti za awali pia zimewekwa mtandaoni zilizo na uhusiano na *Utenzi wa Katirifu* kama vile *Utenzi wa Herekali*.

Mswada tuliutumia katika kufanya utafiti wetu ni ule ulioandikwa na Knappert (1979). Si mswada huu pekee tuliutumia bali tulisoma miswada mingine iliyoandikwa kuhusu *Utenzi wa Katirifu*. Tumeufuata ushauri na mwongozo tuliopewa na wasimamizi wetu. Mwisho tumeyasoma makala yanayohusiana na Uislamu kwa kuwa *Utenzi wa Katirifu* umeandikwa ili kuzungumzia maswala ya dini ya Kiislamu. Kazi hizo zote zimetufaa kuelewa zaidi kazi husika namna ambavyo tumehakiki vipengele hivyo.

1.10 Hitimisho.

Katika sura hii ya kwanza, tumeyaangazia maswala yote ya kimsingi yanayohusiana na utafiti tulioufanya. Maswala hayo ni pamoja na utangulizi, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, msingi wa kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti.

SURA YA PILI.

WAHUSIKA NA UHUSIKA WAO KATIKA *UTENZI WA KATIRIFU*.

2.1 Utangulizi.

Katika sura hii, tumeangazia uhakiki wa wahusika na uhusika wao katika *Utenzi wa Katirifu*. Mwanzo tumefafanua dhana wahusika kwa namna ambavyo inatumika katika fasihi, kisha tumeonyesha migao ya wahusika hao. Wanagawika katika makundi mbalimbali kulingana na sifa zinazotumiwa kuwabainisha. Mifano tuliyoitumia tumeitoa kutoka kwenye *Utenzi wa Katirifu*.

Wahusika ni viumbe wanaoumbwa na mtunzi wa kazi ya fasihi ili wamfae katika kuwasilisha dhamira au ujumbe aliokusudia kwa hadhira inayoweza kuwa wasomaji au wasikilizaji. Katika fasihi simulizi, wahusika huweza kuwa binadamu, wadudu, wanyama, mimea na hata mazimwi. Katika kazi nyingine kuna matumizi ya vibonzo kama vile katika michezo ya watoto.

Wahusika wengi katika tenzi huwa ni watu walio na sifa za kimaadili. Tabia zao hutofautiana katika kuwatambulisha au hutambulishwa na matendo yao na wanayoyasema wahusika wengine kuwahusu. Wahusika katika fasihi ni viwakilishi tu katika ulimwengu halisi wala si lazima sifa zao zifanane kwa namna ya moja kwa moja.

2.2 Uhusika na wahusika.

Uhusika ni mbinu inayotumiwa na mwandishi wa fasihi kuwatambulisha wahusika. Athari inayotolewa na matukio ndiyo huwa na uzito katika fasihi. Athari ya matukio huleta matokeo mengi ya kazi inayowasilishwa. Uhusika pia ni hali ya kufananisha vitendo vya wahusika katika fasihi na viumbe wanaopatikana katika ulimwengu

halisi. Njogu na Chimera (1999) wanasema kuwa wahusika wa zamani walisawiriwa kihalisi. Walifanana kitabia na binadamu waliopatikana katika ulimwengu halisi.

Wahusika hugawika katika makundi mawili makuu kulingana na namna wanavyotokea katika kazi fulani. Kuna wahusika wa kihalisia na wale wa kifantasia. Sifa za mhusika wa kihalisia hushabihiana na zile za binadamu wa kawaida ilhali zile za mhusika wa kifantasia hukosa ukawaida. Fasihi ya kinjozi huelezea kuhusu matukio yasiyo ya kawaida. Mawazo ya kinjozi huwa ya kiwango cha juu kabisa. Sifa hukuzwa kuliko kawaida. Wahusika waliojadiliwa katika utenzi huu wametokea katika hali mbili – hali halisi na ile ya kinjozi. Wahusika waliotokea katika hali halisi ni kama vile: Hasina, Katirifu, Mchungaji na Amri. Ni wahusika wanaoweza kupatikana katika mazingira na hali za kawaida. Matendo yao pia ni ya kawaida.

Wahusika wengine kama vile Mtume Muhammad (S.A.W) na wafuasi wake na Ali si wahusika wa kawaida. Matendo yao hayaingiliani na hali za kawaida ama zinazoweza kutendeka katika hali halisi. Kwa mfano, Ali anaitwa simba. Ni shujaa. Ana uwezo wa kiajabu kwa kuwa anawaua watu wengi mno. Pia, anatumia masaa machache mno katika safari zinazofaa kuchukua siku nyingi.

Hata hivyo, wahusika hao wote wamesaidia mno katika kujengana na kukamilishania ya mtunzi wa *Utenzi wa Katirifu*.

2.3 Mbinu za kuwasawiri wahusika.

Mbinu za kuwasawiri wahusika ni namna wanavyochorwa au kuwasilishwa na msanii. Mbinu hizi tofauti hutokana na mambo kama vile maelezo ambayo wasomaji au wasikilizaji hupewa kuhusu mhusika fulani. Maelezo haya huweza kuwa wazi au fiche, ya kina au hata ya kisaikolojia. Dhamira ya mwandishi husaidia katika

kuwaweka wahusika katika makundi. Kuna wema na waovu kama ilivyo katika ulimwengu halisi.

Usawiri huhusisha majina na matumizi ya lugha zao katika fasihi. Usawiri wa wahusika hutegemea wakati ambapo kazi hiyo ilitungwa. Kwa mfano: baadhi ya wahusika walitumika wakati wa fasihi simulizi. Mbinu mbalimbali hutumiwa kuwaweka wahusika katika makundi. Mbinu zifuatazo zimetumiwa katika *Utenzi wa Katirifu* ili kuwasawiri wahusika waliotumika.

2.3.1 Matendo au matumizi ya mazungumzo.

Maneno yaliyotumika na wahusika huweza kuwakuza wahusika wenyewe. Maneno hayo huzua mgogoro ulio katika kazi fulani ya fasihi ambao utaendelezwa na baadaye suluhisho kupatikana. Wamitila (2002) na Njogu na Chimera (1999) wanasema kuwa mgogoro uliozuka ndio unaochangia pakubwa katika kukuza na kuendeleza dhamira ya mtunzi husika.

Katika *Utenzi wa Katirifu*, tunaelewa baadhi za tabia za wahusika kama vile Hasina kutokana na mazungumzo kati ya Hasina na Katirifu. Hasina anaonyeshwa kuwa mwovu. Anamtaka Katirifu kulipiza kisasi kwa kuwa babake aliuawa kwa uovu wake.

Mgogoro katika *Utenzi wa Katirifu* unaanzia kwenye mazungumzo kati ya Amri na Mchungaji. Amri anasimuliwa yaliyotokea (matumizi ya mbinu rejeshi). Mazungumzo hayo ndiyo yaliyodokeza asili ya vita hivi kati ya Waislamu na makafiri. Amri anadhihirishwa kuwa mpenda dini kwa kuwa hakutaka kuendelea kusikiliza aliyokuwa akisimuliwa kwa kuwa aliona kama kwamba Mtume Muhammad (S.A.W) anaonewa.

2.3.2 Maelezo au masimulizi yanayotolewa na mtunzi / mwandishi.

Katika mbinu hii mwandishi huamua kumpa sifa mhusika kupitia matendo yake, au hata mandhari anapopatikana mhusika huyo. Sifa hizo humfanya msomaji wa kazi husika kukubaliana na mtunzi kuhusu sifa za mhusika huyo. Kwa mfano, maelezo kuhusu Hasina na vitendo anavyotaka Katirifu avifanye moja kwa moja yanabaini sifa za Hasina kama mhusika mwovu. Ali naye anapewa sifa ya kuwa mkali hata akaitwa simba. Neno simba linaonyesha kuwa Ali ni mtu shujaa na asiyeogopa chochote.

2.3.3 Maelezo kutokana na wahusika wengine.

Mtunzi anaweza kutumia mhusika anayeeleza sifa za mhusika mwingine. Maelezo haya huenda yakawa ya kweli au si ya kweli kwa kuwa kwa kiasi kikubwa yanategemea mtazamo wa mhusika binafsi. Ikiwa anampenda atamkuza, na ikiwa ana mwelekeo hasi kumhusu, atamdunisha. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Katirifu*, mtunzi amemdunisha Katirifu kwa kuwa anakusudia kuyatenda mabaya kutoka mwanzoni. Habainishi asili ya kisasi hiki kabla ya kuanza kuandaa vita.

2.3.4 Matumizi ya majina ya kimajazi na lakabu.

Majazi humaanisha ile mbinu ya kuwapa wahusika majina kulingana na vitendo au tabia zao. Hii huweza kumsaidia msomaji kuelewa tabia za mhusika fulani kabla hata ya kuisoma kazi hiyo. Mwandishi atakuwa tayari amekwisha wasilisha tabia ya mhusika kwa wasomaji hivyo kuwakosesha nafasi ya kufanya maamuzi kuhusu mhusika huyo. Katika *Utenzi wa Katirifu* Ali anaitwa simba-Haidari. Jambo hili linaonyesha kuwa ni mtu mkali na hivyo ndivyo inavyobainika katika utenzi wenyewe.

2.3.5 Mbinu ya mgotanisho.

Mwandishi huweza kuwaweka au kuwatumia wahusika wawili au zaidi kwa usambamba. Wanapotumiwa kwa pamoja, tabia zao hueleweka zaidi kuliko wakati anapotumiwa mmoja tukwa wakati mmoja. Sifa zao huweza kulingana au kutofautiana kulingana na nafasi wanayoichukua katika kazi husika. Kwa mfano, Katirifu na Hasina wametumiwa kwa pamoja. Sifa zao zinaonyeshwa kuwa za tamaa kubwa na mwingine kisasi. Yote ni maovu. Kidari na Katirifu wametumiwa kuonyesha wahusika wasiokata tamaa kwa haraka. Inabainika kuwa wameshindwa vitani ila wanaendelea tu kupigana. Hawafi moyo.

2.4 Umakundi wa wahusika.

Katika fasihi, wahusika hudhihirishwa kwa namna mbili. Kuna wahusika halisi ambao hudumu katika mazingira halisi au hali zinazowezekana kulingana na maumbile. Matukio yao huwa ya kihalisia – yanaweza kutokea au kufanyika. Katika utenzi wa Katirifu, wahusika kama vile Hasina, Katirifu, Amri na wengineo ni wahusika halisi.

Pili, kunawahusika wa kinjozi. Hawa si wa kihalisi kwa kuwa matendo yao hayawezeke katika ulimwengu halisi. Hali na matendo yao hukinza yale yanayowezeke katika ulimwengu halisi. Katika *Utenzi wa Katirifu* mhusika Ali anadhihirishwa kuwa mhusika wa kimazingaombwe kwa kuwa matendo yake si ya kawaida. Safari yake humchukua siku chache kuliko ilivyo kawaida ya wahusika wengine. Anawapiga na kuwaua watu wengi sana vitani. Hadhihirishwi kuwa mhusika wa kawaida.

Wahusika hugawika katika makundi mawili: Wahusika wakuu na wahusika wadogo au wasaidizi. Katika sura hii, tumewahakiki wahusika kwa kuzingatia sifa zao, aina na mbinu zilizotumika kuwasawiri.

2.4.1 Wahusika wakuu.

Wahusika wakuu ni wale ambao huwakilisha matukio muhimu katika kazi husika ya kifasihi. Njogu na Chimera (1999) wanasema kuwa migogoro na matendo ya wahusika hawa ndio huisukuma kazi ya kifasihi mbele. Mhusika huyu hawezi kuondolewa kutoka kwenye kazi ya fasihi na akiondolewa basi kazi yenyewe hufa. Kazi yoyote ya fasihi hutegemea pakubwa mhusika mkuu.

Wahusika hawa hutawala kazi ya mtunzi. Dhamira ya mtunzi husika hupitishwa kwao. Matendo makuu huwazingira. Mtunzi huwaunda ili kutekeleza majukumu fulani. Kupitia majukumu wanayotekeleza basi dhamira na maudhui yaliyokusudiwa huwasilishwa. Tumewajadili wahusika hao na majukumu waliyotekeleza katika kuwasilisha dhamira ya mtunzi wa *Utenzi wa Katirifu*.

2.4.1.1 Katirifu.

Utenzi huu umeitwa *Utenzi wa Katirifu* kwa kuwa Katirifu ndiye mhusika mkuu. Katirifu alikuwa na hamu ya kumwoa Hasina kwa kuwa ni mrembo. Hasina anamwambia kuwa ikiwa atataka kumwoa basi awakamate Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali kabla ya kumwoa. Anaingia vitani lakini anashindwa. Hasina anamhimiza kurejea kisha anauliwa. Mtunzi amemtumia mhusika Katirifu kuwasilisha maudhui mengi na pia kuwajumuisha wahusika wengine ambao hawajatajwa moja kwa moja katika utenzi huu.

Katirifu ni mwenye tamaa kwa kuwa tamaa ya kumwoa Hasina kwa sababu ya urembo wake ndiyo inayomsukuma kwenda vitani. Hasina alimwahidi kuwa

akimwua Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali atamwoa. Hasina alitaka kulipiza kisasi kwa kuwa babake aliuliwa na mtume na Ali vitani. Tamaa yake ndiyo inayomsukuma kwenda vitani. Hata baada ya kushindwa, Hasina anamhimiza kurejea tena na huko vitani anauliwa. Mtunzi amemtumia mhusika Katirifu kuonyesha kuwa kuna watu walio na tamaa na tamaa hiyo huwasukuma kutenda maovu. Tamaa hiyo pia huwapeleka watu kwenye mauti bila kufahamu.

Katirifu anaonyeshwa na mtunzi kuwa mhusika mwenye msimamo thabiti. Anapoamua kuwa anataka kumwoa Hasina, haonekani kubadilisha nia yake hata ingawa masharti anayopewa ni magumu. Anajitolea kwenda vitani. Anashindwa, anarejea tena na kuuawa. Matendo hayo yote yanaonyesha msimamo thabiti alio nao kuhusu kumwoa Hasina. Habadiliki kabisa hata baada ya maisha yake kutishiwa na hali iliyokuwa hatari.

Kutokana na msimamo wake huo anaweza pia kuchukuliwa kuwa mwenye mapenzi ya dhati. Anampenda Hasina mara ya kwanza anapokutana naye. Masharti ya kumwoa yanapokuwa magumu, anaendelea kushikilia msimamo wake. Jambo hili linadhihirisha kuwa alimpenda Hasina ndio maana aliamua kufanya hayo yote. Ingekuwa hakumpenda, basi hangeyafanya hayo yote.

Katirifu ni mwenye bidii. Jitihada zake za kujaribu kuwaua Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali zinaonyesha kuwa ana bidii. Ingawa anadhihirishwa kuwa hana uwezo wa kuyafanya hayo anatia bidii kukusanya majeshi yake na kuyaandaa kuingia vitani. Anashindwa lakini anarejea na kutia bidii zaidi ili ampate Hasina kama mkewe. Mwisho, anauawa vitani.

Katirifu anaonyeshwa kuwa mhusika ambaye ni jasiri. Ujasiri wake unatokana na kujitolea kwake kuenda vitani. Katika hali ya kawaida ni wahusika wachache

wanaoweza kukubali kuenda vitani. Hii ni kutokana na hatari inayowakabili walioko vitani hasa kifo. Kwa sababu ya tamaa na mapenzi aliyo nayo Katirifu kwa Hasina, anakubali kuenda vitani. Hii inaonyesha kuwa alikuwa jasiri.

Katirifu pia ana sifa ya utiifu. Anayatii masharti yote aliyopewa na Hasina. Ili apate kumwoa, Hasina anamwambia aandaie vita ili kulipiza kisasi kwa niaba ya babake aliyeuawa vitani. Anajiandaa na kuandaa makundi yake na kuenda vitani. Alishindwa akarejea kwa Hasina. Anaitii amri ya pili ya Hasina ya kurejea vitani na huko anauliwa.

Katirifu ni mhusika aliye rahisi kushawishika. Tamaa aliyo nayo kwa Hasina ndiyo inayoufanya moyo wake kushawishika kwa urahisi kuenda vitani. Asingekuwa rahisi kushawishika basi asingeenda vitani kuyatimiza matakwa ya Hasina. Sifa hiyo ndiyo inayompeleka kukutana na mauti yake.

Usawiri wa Katirifu umeonyeshwa kupitia kwa matendo yake mwenyewe kama mhusika. Vitendo anavyovifanya vinaonyesha wazi tabia yake. Tendo la kukubali kuenda vitani linambaini kama mtu aliye na msimamo ulio thabiti. Si hilo tu, kitendo chake cha kukubali kurejea vitani kinaonyesha kuwa hafi moyo kwa urahisi.

Pili, mtunzi amewatumia wahusika wengine ili kumkuza na pia kumdunisha Katirifu. Kupitia kwa Hasina, Katirifu amekuzwa kisifa na kuonyeshwa kuwa mhusika mwenye msimamo thabiti. Msimamo wake katika kufanya maamuzi unaonyeshwa kupitia kwa matendo na mazungumzo yake na Hasina.

Mhusika mwingine aliyemkuza na vilevile kumdunisha Katirifu ni Kidari. Kupitia matendo na mazungumzo ya Kidari na Katirifu, Katirifu anaonyeshwa kuwa hana utu kwa upande mmoja, kwa upande mwingine anaonyeshwa kuwa ana msimamo thabiti.

Kidari ameumizwa vitani na hata kukatwa masikio lakini Katirifu hamwonei huruma ila tu anamhimiza kurejea vitani.

Katirifu ni mhusika mkuu katika kazi hii kwa kuwa vita katika utenzi huu vinasababishwa naye. Vita hivi ni maudhui makuu katika utenzi huu kwa kuwa vimetamalaki kutoka mwanzo hadi mwisho wa utenzi. Dhamira kuu ya kazi hii ambayo ni kutetea na kuleta usawa katika jamii imepitishwa kupitia kwake. Hadhihiriki katika kazi nzima. Anaonekana mwanzoni, kati na vita vinapoisha. Anapokufa kazi ya mtunzi inaonekana kukamilika na suluhisho la mgogoro uliokuwepo kupatikana.

Kitabia, Katirifu anaonyeshwa kuwa mhusika bapa kwa kuwa ana tabia moja kutoka mwanzo hadi mwisho. Pili, habadilishwi na hali ya kimaisha inayomzunguka. Yuko katika hatarikubwa lakini hataki kuacha vita hivyo. Hali za wahusika wengine vilevile hazimbadili kwa mfano alipoona Kidari amekatwa masiko hakumkataza asirejee vitani. Anamhimiza kuendelea na vita. Inakuwa vigumu kuitabiri hali ya Katirifu kwa kuwa haonyeshi athari ya hisia za aina yoyote ile. Katirifu anamwambia Kidari:

Katirifu kamwambia
Rudi tena hiyo ndia
Na hasara ungangia
Ndiwe shujaa shururi (ubeti363)

2.4.1.2 Hasina.

Hasina ni mwanawe mhusika mmoja aliyeuawa katika vita vya Badri. Babake alikuwa tajiri kupindukia kutokana na mali aliyomwachia Hasina kurithi. Hata hivyo, anadhihirishwa kuwa alikuwa mwovu. Ni mwanamke anayebainishwa na mtunzi kuwa tajiri sana kutokana na urithi alioachiwa na babake. Haya ni maelezo yanayotolewa na mchungaji kwa Amri.

Hata hivyo, amefuata njia kama zile za babake kwa kuwa ni mwovu. Anataka kulipiziwa kisasi dhidi ya Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali kwa niaba ya babake.

Hasina ni mtenda maovu. Kutokana na mazungumzo ya Mchungaji na Amri, tunamwelezwa kuhusu tabia ya babake Hasina. Mchungaji anaelezea kuwa babake Hasina alikuwa mtenda maovu naye Hasina alifuata tabia kama hiyo. Anasema:

Yule mtu mpotofu
Na mambo yake dhaifu
Kimukanya mwongofu
Hatta siku ya Nushuri (ubeti 26)

Na mwanawe umufuwete
Maovu uyakemete
Ujingani akatate
Akiliye si kathiri (ubeti 27)

Uovu wa Hasina pia unadhihirika anapomtaka Katirifu kwenda kuwakamata Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali. Katirifu anakubali kufanya hivyo ili posa yake ikubalike na Hasina. Matamshi yake yanaonyeshakuwa alitaka wauliwe ili hata wasiwaone tena watoto na wake zao. Hasina anasema:

Kamba nenda kamteke
Na Ali umushike
Zijana zao na wake
Wasiwandike nadhari (ubeti 32)

Hasina ni mwenye kisasi. Vita vinavyotokea katika utenzi huu vinatokana na Hasina kutaka kulipiza kisasi kwa Ali na Mtume Muhammad (S.A.W). Hii ni kwa sababu wao ndio waliomwua baba yake. Ana matumaini makuu kuwa atafaulu katika kulipiza kisasi hicho. Anamtumia Katirifu katika kuandaa na kutekeleza hayo ila anashindwa. Katirifu aliyetegemewa anauawa vitani. Hasina anasema:

T`arudia neno langu
Nikariri ulimi wangu
Kiswaswi kya bwana wangu
Ndilo liwelo kathari (ubeti 391)

Hasina ni mhusika mwenye msimamo thabiti. Nia yake kutoka mwanzoni mwa utenzi huu ni kuwaona Ali na Mtume Muhammad (S.A.W) wakiuliwa. Katirifu anaenda vitani, anashindwa na kurejea. Hatari ya vita haimfanyi Hasina kuabadili msimamo wake na kuwa na woga kuwa vita husababisha hata maafa. Mwisho, anamlaumu Katirifu kuwa ndiye aliyejisababishia kifo.

Hata ingawa mtunzi hajakwonyesha Hasina waziwazi akishiriki katika vita, Hasina ana ujasiri mkubwa wa kumtaka Katirifu kuwaua Ali na Mtume Muhammad (S.A.W). Mhusika asiyekuwa na utu ndiye atakayemtaka mwenzake kuuawa. Ujasiri na ukosefu wa utu unadhihirishwa na Hasina kwa kiwango kikubwa.

Usawiri wa Hasina umeonyeshwa kupitia kwa wahusika wengine kama vile mchungaji. Ni kupitia maelezo ya mchungaji tunapopata kuelewa tabia ya Hasina. Hasina ndiye anayesema kuwa Katirifu akiwaua Ali na Mtume Muhammad (S.A.W), hayo yatakuwa mahari ili apate kumwoa. Mazungumzo kati ya Hasina na Katirifu yanaonyesha baadhi ya tabia za Hasina kama mhusika mwenye msimamo thabiti na katili. Hivyo, Katirifu anasaidia kuonyesha kuwa Hasina hakuwa mhusika aliyekuwa rahisi kushawishika. Habadilishi mawazo yake anaporudi vitani kwa kuwa alijua fika kwamba angeuawa.

Hasina ni mhusika bapa kwa kuwa haonekani kubadilika kutoka mwanzoni hadi mwishoni mwa utenzi huu. Msimamo alio nao wa kuwataka Ali na Mtume Muhammad (S.A.W) wauliwe ndio anaokuwa nao hadi mwishoni. Haonyeshi kuwa na woga unaotokana na hatari inayokuwa vitani kama vile mauti. Kifo kinaonyeshwa kuwa kitendo cha kumletea furaha mradi haja yake imetimizwa. Hatimaye, anamlaumu Katirifu baada ya kifo chake akisahau kuwa yeye ndiye aliyekuwa sababu kuu (ubeti 413).

Mtunzi amemtumia Hasina kuonyesha kuwa kuna baadhi ya watu wasiobadili misimamo yao kwa urahisi hata hali zinazowakabili zinapobadilika na kuwa ngumu zaidi. Kwa mfano, Hasina angeikubali posa ya Katirifu alipoona kuwa Katirifu alikuwa ameshindwa vitani na hali iliyomkabili ilikuwa inahatarisha maisha yake. Pili, Hasina ametumiwa kama kitambulisho cha wanawake waovu katika jamii hiyo.

2.4.1.3 Mtume Muhammad. (S.A.W)

Mtume Mohammad (S.A.W) ni mmoja kati ya wahusika katika *Utenzi wa Katirifu*. Alimwua babake Hasina katika vita vya Badri – vita kati ya waislamu na makafiri. Mtume Muhammad (S.A.W) alishiriki katika vita hivi kwa kuwa hakupenda maovu na hivyo Hasina anataka kulipiza kisasi.

Mtunzi anamdhihirisha Mtume Muhammad (S.A.W) kama mpenda haki. Toka mwanzoni hadi mwishoni kuiona jamii isiyokuwa na maonevu hata kidogo. Mtume Muhammad (S.A.W) hakupenda maovu ndio maana amesimama kidete na kushiriki katika vita ili kuitetea jamii hii ya wanyonge. Mauaji ya babake Hasina ndiyo yanayoleta kisasi na vita vinavyopiganwa hivi sasa. Hata ingawa anamwamrisha Bilali kutangaza vita, anataka kuona mazuri yakitokana na vita hivyo. Anatoa ahadi kwa watakaoshiriki katika vita hivyo kuwa hawatachomwa na moto kesho ahera. Anamwambia Zai'di:

Zaidi bunu Katibu
Na wengine ashabu
Kawadhamini Habibu
Kesho kwepuka na nari (ubeti 203)

Ni mtu aliyewajibika na wa kutegemewa. Katika vita vya kwanza alipigania haki ya wanajamii. Babake Hasina aliuawa katika vita hivyo ambavyo vinaleta kisasi cha sasa. Katika vita vya kwanza alipigana ili kuleta mabadiliko na usawa katika jamii

hiyo. Ameuthamini utu na usawa na kutaka kuona watu wakiishi katika hali nzuri. Ametumiwa na mtunzi kusimamia ukweli na haki.

Ametumiwa na mtunzi kuonyesha kuwa hata ingawa kuna waovu wengi katika dunia hii, kuna baadhi wanaoona maonevu hayo na kutaka ulimwengu wenye haki na usawa kwa wote. Vita hivyo anaviandaa ili kukomesha maovu ya babake Hasina na anafaulu. Katika vita vya pili pia anafaulu. Mtume Muhammad (S.A.W) amewekwa katika mazingira halisi ili kuonyesha kuwa haya ni mambo yanayowezekana katika ulimwengu halisi.

Mtume Muhammad (S.A.W) amesawiriwa kupitia kwa mazungumzo kati ya mchungaji na Amri. Katika mazungumzo yao, Mtume Muhammad (S.A.W) anaonyeshwa kuwa na huruma na mapenzi kwa watu wake. Amri anamwonyesha Mtume Muhammad (S.A.W) kumiliki sifa hiyo kwa kusema yafuatayo

Upuzi wa m`tu jura
Asokuwa na fikira
T`umwa mwenye maghafura
Huwaye kumdhifiri? (ubeti 51)

Matamshi yake binafsi yanadhihirisha baadhi ya tabia zake. Anapopata ripoti kutoka kwa Amri kuwa Katirifu alikuwa akijiandaa kwa vita, anamwita Bilali na kumwambia atangaze vita. Katika vita hivyo anatoa ahadi kwa watakaoshiriki. Anasema kuwa atawaepusha kutoka kwenye moto.

Kutokana na sifa ya kutobadilika kutoka mwanzoni hadi mwishoni mwa utenzi, Mtume Muhammad (S.A.W) ana sifa za mhusika bapa. Hakuna hali yoyote inayombadilisha. Katika vita vya kwanza alipigana kwa sababu ya maovu. Katika vita vya pili anabakia kuwa na msimamo huo.

Hata hivyo matendo mengine ya Mtume Muhammad (S.A.W) si ya kawaida. Matendo yake hayaingiliani na hali za kawaida ama zinazoweza kutendeka katika

hali halisi. Kwa mfano, safari ya siku nyingi inamchukua masaa machache tu ama anafika katika sehemu za vita bila msimulizi kuelezea alifika vipi.

2.4.2 Wahusika wasaidizi.

2.4.2.1 Amri.

Kulingana na usimulizi unaotolewa na mtunzi wa utenzi huu asili ya Amri ilikuwa ni Myahudi aliyebadili dini akaamua kumfuata Mtume Muhammad (S.A.W). Alihama nchi yake na kuwaacha mkewe na wanawe. Aliiacha dini yake kwa kuwa aliitwa na Mwenyezi Mungu akafuate Uislamu. Mtunzi anasema:

Kwalina m`tu Yahudi
Moyo wake ukarudi
Kaelekea Muhamadi
T`umwa wetu mansuri

Na mkitaka isimu
Yinale mulifahamu
Isimule ma`alumu
Aliitwa Amri (ubeti 14-15)

Anasimuliwa kisa kuhusu Hasina na Katirifu na mchungaji Mwarabu aliyekutana naye jangwani. Anamsikiliza kwa makini kisha anamwambia mchungaji aache kusimulia kwa kuwa alikuwa akimkasirisha kwa maneno yale. Anapotajiwa Mtume Muhammad (S.A.W) kukamatwa, anamwambia mchungaji aache kabisa kusimulia kisa hicho. Hapa anadhihirishwa kuwa mwenye hasira na imani ya hali ya juu katika dini ya kiislamu kwa sababu hakutaka kusikia kuwa kiongozi wa dini hiyo amekatwa.

Anaendelea na safari yake hadi Madina anapokutana na Mtume Muhammad (S.A.W) na wafuasi wake msikitini. Baada ya salamu, anawaeleze ayaliyojiri njiani. Papo hapo Mtume Muhammad (S.A.W) anamwita Bilali na kumwambia atangaze vita.

Amri ni mwenye msimamo thabiti. Anaamua kuiasi dini yake na kufuata Uislamu. Kitendo hicho kinamfanya kuiacha nchi pamoja na jamii yake na kufunga

safari kuelekea Medina. Si mhusika wa kubadili misimamo, alifanya uamuzi kuufuata msimamo wake.

Amri ni mhusika anayependa na kutetea haki. Mchungaji anapomsimulia Amri mipango ya Katirifu ya kutaka kuwaua Ali na Mtume Muhammad (S.A.W), haonekani kukubali mpango huo kwa kuwa anaelewa kuwa babake Hasina aliuliwa kutokana na utetezi wa haki wa Ali na Mtume Muhammad (S.A.W). Anashikwa na hasira na kuondoka. Anaenda mpaka Medina na kuwelezea Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali aliyokusudia kuyatenda Katirifu. Hapo pia anadhihirishwa kuwa si mvumilivu kwa kuwa anamwambia mchungaji aache kusimulia. Anamwambia:

Sipendi kuipulika
Basi habari zuwika
Nenda zangu kwa mmaka
Kipenda mulatahari (ubeti 32)

Usawiri wa mhusika Amri umefanywa kupitia kwa mbinu ya mazungumzo. Sifa zake zinabainika kwa wasomaji kutokana na mazungumzo kati yake na mchungaji. Katika mazungumzo hayo anabainika kuwa mwenye hasira na mwenye mapenzi katika dini ya Uislamu aliyoichagua. Mapenzi hayo yanaonyeshwa kupitia kwa kitendo chake cha kuenda mpaka Medina alikokuwa Mtume Muhammad (S.A.W).

Kutokana na maelezo ya mtunzi kuhusu Amri anaonyeshwa kuwa mhusika duara. Uduara wake unatokana na kuwa anaweza kubadilika kulingana na hali iliyopo kwa wakati huo. Kwa mfano, anaamua kuiacha dini yake kabisa na kisha kufuata Uislamu. Haonekani kubadili nia yake. Anaiacha jamii yake na kuushika Uislamu. Mchungaji anapoelezea nia ya Katirifu kumhusu Mtume Muhammad (S.A.W) anashikwa na ghadhabu mno. Anapanda farasi wake na kuondoka mbio.

Mtunzi wa *Utenzi wa Katirifu* amemtumia mhusika Amri kuonyesha kuwa wahusika wanaweza kubadilika na kuwa imara katika misimamo yao. Pili, amemtumia kama

kielelezo cha dini yaani kuna wale wanaoweza kuacha dini zao. Asili ya Amri ilikuwa Ukristo kwa kuwa alikuwa Myahudi. Anaamua kubadilika na kuwa Mwislamu kamili.

2.4.2.2 Mchungaji.

Mchungaji amepewa nafasi ndogo sana katika kuwasilisha maudhui ya mtunzi huyu. Hata hivyo, anayoyawasilisha yanatoa mchango mkubwa katika kuendeleza hadithi nzima. Baadhi ya sifa zinazomtambulisha ni kama vile utiifu. Anapokatazwa aache kusimulia anaacha mara moja. Mhusika huyu amesawiriwa na msimulizi kuwa alikuwa mtu maskini. Alikuwa mtu wa tabaka la chini kwa kuwa alikuwa mchungaji.

Mtunzi anaeleza:

Na mtu`ye ni mtunga
Uvee nguwo za Manga
Papo kipeka maninga
Uiwene kuu dari

Kyali kyungu `adhimu
Katika wangwa fahamu
Na inde yali kaumu
Isokuwa na kadiri (ubeti 19-20)

Kupitia kwake tunapata kuelewa tabia za wahusika Hasina, Katirifu na Amri. Anaieleza tabia ya Hasina kuwa ya uovu, Katirifu anaonyeshwa kuwa na tamaa iliyozidi kiwango naye Amri kuonyeshwa kuwa mwenye hasira.

Kupitia kwake mtunzi ameelezea kuhusu vita vilivyoandaliwa na vilivyokuwa kati ya waislamu na makafiri. Vita hivyo vinatawala hadithi nzima.

2.4.2.3 Ali.

Ali ni shujaa aliyeshiriki katika vita vya kwanza wakati babake Hasina alipouawa. Mchungaji anaelezea kuwa Hasina anataka kulipiza kisasi kwake. Anataka Ali na Mtume Muhammad (S.A.W) wauawe kwa kuwa walimwua babake. Katika vita hivi

anadhihirishwa kuwa mhusika muhimu kwa kuwa ndiye anayefika vitani na kuwaua watu wengi mno. Vita hivyo vinaisha anapomwua Katirifu.

Sifa zifuatazo zinamtambulisha mhusika Ali. Ali ni mwenye hasira. Anapokuwa vitani anaonyesha hasira kwa namna ambavyo anapigana. Msimulizi anasema kuwa hasira aliyokuwa nayo ilimfanya kuutupa mkuki mmoja tu na kumuua Kidari. Katirifu anapona kuwa Kidari ameuawa alishikwa na woga na kurejea kwa Hasina.

Hasina anamwambia arejee vitani. Msimulizi anasema:

Akenda kayahatibu
Ya imamu ma`ayubu
Alii kataghadhabu
Akapotoa sadiri

Asipende kupulika
Kisa neno kutamuka
Upangawe kumwandika
Ukenda nt`i dhahir

Kidari na zake fili

Akawatinda pawili (ubeti 367-369)

Ali anaonyeshwa kuwa mhusika mtiifu. Alipokuwa amelala anaota ndoto kuwa Mtume Muhammad (S.A.W) alikuwa vitani na kuwa alihitaji msaada wake katika vita hivyo. Atika anashangazwa na matukio ya Ali kuzungumza na Mtume Muhammad (S.A.W) akiwa ndotoni. Anapoamka anaitii amri ya Mtume Muhammad (S.A.W) kwa kuwa anaondoka kuenda vitani. Msimulizi anasema:

Haidari katamuka
Nitanenda kuyitika
Wahadahu la shirika
Alipendalo kujiri (ubeti 271)

Ali ni katili. Ukatili wake unaonyeshwa katika kisa cha kwanza ambapo pamoja na Mtume Muhammad (S.A.W) walimwua babake Hasina. Matendo yake anapokuwa vitani yanaonyesha kuwa alikuwa mtu katili kwa namna ambavyo alikuwa akiwaua watu. Msimulizi anasema kuwa alikuwa akiwavunja vichwa kwa kutumia Dhu

L`Fikar (upanga). Angemwua mtu kwa kumtazama tu au hata kwa kumwuma kwa meno yake.

Ali ni jasiri kwa kuwa anakubali kuenda kupigana vitani. Haonyeshi uoga unaotokana na athari za vita kama vile kifo. Anapoitwa kuenda vitani anautikia mwito bila ya kuuliza maswali yoyote. Anaposhauriwa na shangaziye Atika aende usiku ili maadui zake wasimwone, anakataa na kuifanya safari hiyo mchana.

Msimulizi anasema:

Atika amwambiziye
Linda usiku ungiye
Wamaka wasisikiye
Wakaya kukuhasiri

Haidari kahuluhu
Akamwambia ummuhu
Hapana munena uhu
Wamaka kunijasiri (ubeti 274-275)

Kutokana na lakabu aliyopewa Ali, inaonyesha kuwa alikuwa mhusika shujaa na aliyetegemewa sana katika kufanya maamuzi vitani. Usawiri wake umeonyeshwa kupitia kwa vitendo na mazungumzo yake. Matendo yake ndiyo yanayompa sifa anazozimiliki.

Pili, wahusika wengine kama vile mchungaji wamesaidia katika kumsawiri mhusika Ali. Ni kupitia kwa mazungumzo ya Amri na mchungaji tunapopata kuelewa asili ya kisasi cha sasa. Vita vya kwanza vilikuwa ni vya kuleta haki na usawa katika jamii hii na Ali alishiriki. Hasina pia anambainisha Ali kwa kumpa sifa ya ukatili kwa sababu alimwua babake.

Maelezo ya msimulizi pia yamesaidia katika kuzipambanua sifa za Ali. Msimulizi amempa lakabu kama vile Simba. Lakabu hii inaonyesha sifa za kikweli za Ali. Ali ni mhusika bapa kielelezo. Anazibadili tabia zake kulingana na hali inayoikumba jamii husika. Kwa mfano, katika utenzi huu haonekani kutoka mwanzoni kwa kuwa

jamii iliishi vizuri. Kwa sababu ya maonevu ya babake Hasina, anamwua. Katika vita vya pili, anakuja kuikomboa jamii hii kwa kuwa vita vya Katirifu vinasababishwa tu na tamaa ya mhusika Katirifu.

2.4.2.4 Babake Hasina.

Babake Hasina ni mhusika tunayeonyeshwa kupitia mbinu rejeshi. Hata hivyo kutokana na maelezo yanayotolewa na mchungaji kwa Amri, tunapata kuelewa baadhi ya sifa za mhusika huyu. Alikuwa mtovu wa maadili kwa kuwa msimulizi anaeleza kuwa Hasina alifuata tabia za babake. Jumba na mali aliyomwachia Hasina yanaonyesha kuwa alikuwa tajiri. Hata hivyo, mtunzi anaendelea kusema kuwa alikuwa amezungukwa na tabaka lililokuwa la chini. Hiyo inamaanisha kuwa hakujishughulisha na maskini katika jamii yake.

Usawiri wa mhusika huyu umeonyeshwa tu kupitia kwa mchungaji kwa maelezo anayoyatoa kwa Amri. Ni mhusika bapa kwa sababu ya tabia ya Hasina. Hakutaka kubadilika na kuacha unafiki kwa kuwa msimulizi anasema kuwa Hasina alifuata tabia za babake.

2.4.2.5 Kidari.

Kidari alikuwa mateka Katirifu aliyemtegemea mno katika kupigana vita hivi. Anaonyeshwa kuwa mhusika jasiri kwa kuwa alikuwa katika mstari wa mbele vitani. Utiifu wake pia unaonyeshwa kwa kutii amri ya Katirifu ya kurudi vitani. Hata hivyo, anauliwa na Ali. Kidari ni mmoja kati ya wahusika wadogo waliotumiwa katika utenzi huu. Ametumiwa kumjenga na kumkamilisha mhusika Katirifu katika utenzi huu. Kidari amesawiriwa kupitia kwa wahusika wengine katika utenzi huu. Katirifu anaonyesha kuwa Kidari alikuwa mtiifu kwa kuwa alitii amri zake.

2.5 Hitimisho.

Katika sura hii, tumehakiki wahusika na uhusika wao. Tumefafanua maana ya dhana wahusika na uhusika. Kisha tumeangalia mbinu ambazo hutumiwa katika kuwasawiri wahusika zikiwemo: maelezo ya msimulizi au mwandishi, maelezo ya wahusika wengine, matumizi ya matendo au mazungumzo, matumizi ya majina ya kimajazi na lakabu na ulinganuzi au mgotanisho wakati wahusika wawili wanapotofautishwa.

Wahusika hawa wamesaidia mno katika kuwasilisha maudhui ya mwandishi. Kupitia hisia za wahusika hawa, mambo mengi yamewasilishwa. Wahusika hao wamesaidiana katika kukamilisha dhamira na maudhui ya mwandishi.

SURA YA TATU.

TASWIRA, DAYALOGIA NA TAMATHALI ZA USEMI.

3.1 Utangulizi.

Lugha hugawika katika sehemu mbili kuu – lugha ya kutamkwa na ile ya kimaandishi. Hivyo ni viwango vya fonetiki na fonolojia katika isimu. Katika kiwango cha maandishi, lugha huweza kubadilishwa kimatamshi au kimaandishi. Alama za uakifishi pia hutumiwa ili kuleta maana fulani iliyokusudiwa.

Lugha huwa na mchango muhimu katika kazi yoyote ile ya fasihi. Lugha ndiyo hutofautisha fasihi na sanaa nyingine kama vile: uchoraji, uchongaji na ufinyanzi. Senkoro (1982) anasema kuwa lugha katika fasihi ndiyo malighafi ya kuundia sanaa hiyo. Sanaa nyingine hazitumii lugha kama malighafi yake. Lugha hutumiwa kuelezea kuhusu yanayotendeka katika jamii fulani kwa njia ya kibunifu.

Kimsingi, lugha huweza kuimarisha au hata kudunisha mawasiliano. Iwapo imetumiwa vizuri basi inaimarisha na ikitumika vibaya basi itadunisha mawasiliano. Lugha ikitumika vyema basi ujumbe huweza kumfikia msomaji au msikilizaji kwa njia nzuri na yenye kueleweka.

Lugha hutoa mchango mkubwa katika fasihi kwa kuwa fasihi ni lugha. Wamitila (2003) anasema kuwa lugha huweza kubainika moja kwa moja au kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja. Uwasilishaji wa dhamira na maudhui hutegemea pakubwa namna lugha ilivyotumika.

Wamitila (2008) anasisitiza mambo yafuatayo kuwa muhimu zaidi katika uhakiki wa mtindo katika fasihi: lugha ya kitamathali, uteuzi wa mtindo, usimulizi, mtazamo na itikadi, muwala, mshikamano na mazungumzo. Tumezijadili mbinu za lugha tukijikita kwenye mifano kutoka kwenye *Utenzi wa Katirifu*.

3.2 Taswira.

Taswira ni maelezo yanayojenga picha ya hali au jambo akilini mwa msomaji au msikilizaji. Mbinu za tashibihi na sitiari husaidia mno katika kujenga taswira. Taswira humsaidia pakubwa msomaji au msikilizaji katika kuelewa mandhari na vitu vinavyoonekana. Hutilia mkazo au msisitizo kauli zilizokwisha kutolewa.

Kuna taswira ya mwandishi wa utenzi huu anapoanza kuiandika kazi hii. Anaomba vifaa ili apate kuiandika kazi hii. Anaomba aletewe kalamu na karatasi ya Shamu na wino mzuri. Anasema kuwa wino huo uwe mwekundu na uwe ndani ya chupa nzuri. Maelezo haya yanachora picha kamili ya namna ambavyo matayarisho yalifanywa.

Maelezo pia yanatolewa kuhusu jumba lile lililokuwa jangwani. Taswira hiyo inaonyesha kuwa jumba lile halikufaa kuwa mahali hapo kwa sababu ya ukubwa na uzuri wake. Jumba hilo lilikuwa limezungukwa na watu waliokuwa wa tabaka la chini. Ukubwa na uzuri wake ndio unaomfanya Amri kutaka kujua mmiliki wake.

Kyali kyungu adimu
Katika wangwa fahamu
Na inde yali kaumu
Isokuwa na kadiri (ubeti 20)

Msimulizi pia ametoa maelezo ya Medina. Amri alipofika pale, palikuwa na lango kubwa na walinzi. Anapewa nafasi ya kuingia na mlinzi huyo. Ua wa sehemu hiyo ulikuwa umeshikana vizuri na hakuna aliyeweza kuona ndani. Maelezo haya yanatupa picha kamili ya namna sehemu hii ilivyoonekana.

Vitani Kidari anakatwa masikio kabla ya kuuawa. Kabla ya hayo kujiri, alikuwa akijisifu kuwa hatamuweza. Msimulizi anaeleza kuwa Kidari alikuwa ametumia dawa ya kulevya. Majibizano kati yake na Ali yanamkasirisha Ali. Kidari anashikwa na aibu na baadaye anauawa akiwa na wapiganaji wengine.

Mtunzi anaelezea namna uso wa Mtume Muhammad (S.A.W) ulivyoonekana wakati alitembelewa na Amri. Namna wafuasi walivyojipanga, alivyowasalimia na kuwafahamisha njama ya Katirifu. Anasema uso wake uling'aa na kuonekana mwenye haiba. Anasema:

Kungia kwake madani
Akenda musikitini
Alimuwene Amini
Uso uzingiye nari (ubeti56)

Omar Bin Omayya anaporejea anatifua vumbi ambalo linafanya jua kutoweka. Hata waliokuwepo wanashindwa kupumua. Mtunzi anaeleza:

Vumbi likiwafulia
Kama kwenenda kwa jua
Kama lisikupumua
Walandishiye nadhari (ubeti 58)

Maelezo hayo yanatoa taswira kamili ya namna ambavyo aliingia mahali pale. Vita vinapoanza mtunzi anatupa picha ya namna vita hivyo vilivyokuwa vikali. Anasema hakuna ndege aliyeimba au wa kula mizoga ilionekana kana kwamba mbingu zilikuwa zinaanguka. Hiyo inaonyesha picha ya vita vilivyoanza kwa ukali mno (ubeti248).

Kuna taswira inayotolewa kuhusu maisha baada ya vita. Mali yote yanakusanywa na kupelekwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W) ili apate kuyagawa kwa waliosalia. Mikufu ya dhahabu, bangili, nguo na mashati vilipelekwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W). Alivigawa vitu hivyo kwa wake na waume waliokuwepo.

3.3 Dayalojia.

Dayalojia ni mazungumzo baina ya wahusika. Mwanzoni mwa utenzi, kuna mazungumzo kati ya Amri na Mchungaji. Amri anapouliza kuhusu nyumba ile nzuri iliyokuwa jangwani (ubeti 22-30). Kupitia kwa mazungumzo yao, mtunzi anaelezea

kuhusu Katirifu na matukio yote kumhusu. Tabia ya Hasina pia inabainishwa katika mazungumzo hayo.

Pili, Katirifu na Hasina wanazungumza kuhusu posa na mahari ambayo Katirifu angelipa. Katika mazungumzo hayo, Katirifu anatoa wazo la kuandikiana mkataba ili Hasina asiye akaubadili msimamo wake baada ya Katirifu kuwaua Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali. Ni katika mazungumzo haya tunapata kuelewa sababu ya kisasi cha Hasina.

Amri anapofika Medina, kunakuwa na mazungumzo kati yake na Mtume Muhammad (S.A.W). Mtume anamwambia amwelezee yote yaliyotokea kule machungani (ubeti 66). Amri anaelezea kuhusu walichokuwa wamekipanga Hasina na Katirifu. Mambo hayo yote yanaelezwa kwa mbinu rejeshi.

Hasina naye anashiriki mazungumzo anapokutana na Katirifu (ubeti78). Anamwambia Katirifu alipize kisasi kwa niaba ya babake aliyeuliwa na Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali kwa sababu ya uovu wake. Katika mazungumzo Hasina anakataa posa ya Katirifu hadi Ali na Mtume Muhammad (S.A.W) watakapouliwa.

Ali anaota ndoto. Anapoamshwa na shangaziye, anamwelezea kuhusu yaliyofanyika ndotoni. Katika ndoto hiyo Ali anaitwa na Mtume Muhammad (S.A.W) kwenda vitani. Anaitikia mwito huo katika mazungumzo kati yake na shangaziye (ubeti 271). Atika anamshauri asafiri usiku lakini Ali anakataa na kusema kuwa atasafiri mchana ili makafiri wamwone. Hata hivyo, mazungumzo hayo si ya moja kwa moja kwa kuwa kisa hiki kinasimuliwa kupitia kwa mbinu rejeshi.

3.4 Tamathali za usemi.

Senkoro (1980) anafafanua tamathali za lugha kuwa ni maneno, sentensi au misemo inayotumiwa na wanafasihi kuwasilisha kazi zao. Mbatia anaelezea tamathali za

usemi kuwa ni ukiushi wa kimakusudi katika maana na mpangilio wa maneno. Mpangilio huu huweza kuibua maana mpya ama kusisitiza tu maana iliyopo. Wamitila (2000) anasema tamathali za usemi ni maneno kama vile tashibihi, tashihisi, takriri n.k. Katika utafiti huu ufafanuzi wa Wamitila na Mbatia umetufaa zaidi katika kuhakiki mtindo katika *Utenzi wa Katirifu*. Mwandishi wa utenzi huu ameibadili lugha kimakusudi ili ama asisitize ujumbe au awasilishe ujumbe ulioko.

3.4.1 Maswali ya balagha.

Maswali ya balagha ni maswali yanayoulizwa ila hayahitaji majibu. Maswali haya hayamhitaji msomaji au msikilizaji kufikiria ili kupata jibu la swali hilo. Jibu huwa limo akilini mwa anayeulizwa au anayesoma kazi husika au huwa tayari analijua. Hisia za ndani au mawazo ni kulifanya jambo fulani kuonekana wazi kwa hadhira au kwa msomaji na kinachozungumziwa katika swali hilo kuangaliwa kwa makini. Hilo ni jambo linalofaa kuwekwa bayana. Maudhui fulani pia huwezwa kuwasilishwa kwa maswali haya.

Baadhi ya wahusika katika *Utenzi wa Katirifu* wameuliza maswali haya kwa nia ya kuwachochea wanaolengwa au kuonyesha umuhimu wa kauli iliyotolewa mwanzoni mwa mazungumzo husika. Tumehakiki maswali ya balagha huku tukitoa mifano kutoka kwenye *Utenzi wa Katirifu*.

Amri anashikwa na ghadhabu anaposimuliwa kuhusu mpango wa Katirifu wa kumwua Mtume Muhammad (S.A.W). Anamwambia mchungaji aache kusimulia na kuuliza swali:

Upuzi wa mtu jura
Asokuwa na fikira
T'umwa mwenye maghafura
Huwaye kumdhifiri? (ubeti 51)

Hapa Mtume Muhammad (S.A.W) anadhihirishwa kuwa mwenye kushinda kila mtu. Anauliza ili kwamba kudharau Katirifu kuwa hamwezi kwa kuwa yeye anamweza kila mtu.

Mtume Muhammad (S.A.W) anawauliza wafuasi wake swali. Anaulizia ni yupi kati yao aliyefika Isibani. Ni nani anaweza kutafuta umati huo wa makafiri.

Upi asuhabu, nyani
Mwenye kwenda Isibani
Kunipatia yakini
Kaumu yao kaffari? (ubeti 129)

Anauliza swali hili huku akijua kuwa wafuasi wake walikuwa wanaifahamu Isibani iliko na walikuwa tayari kuenda huko.

Umar bin Umayya pia anamwuliza Mtume Muhammad (S.A.W) swali. Baada ya kupanda farasi wake anamwuliza Mtume Mohammad (S.A.W) alichokitaka.

Kalingana farasini
Kenda mbee za Amini
Kamba T'umwa wapendani
Upendalo ni hubiri? (ubeti 163)

Omar anauliza swali baada ya kurejea kutoka alikotumwa. Majeshi ya Katirifu yalikuwa yashajikusanya akauliza mtume na wafuasi walikuwa wanasubiri nini ilhali majeshi ya Katirifu yalikuwa yamejikusanya tokea jioni iliyotangulia.

Wahalifuo Mannani
Wayiye tangu iyon
Basi T'umwa tulindani
Walipo kutodhihiri? (ubeti153)

Maswali ya balagha yamejadiliwa katika kiwango cha grafonolojia katika nadharia ya umitindo. Alama ya kuulizia imetumiwa katika maandishi ili kuonyesha kuwa kuna maswali yameulizwa. Mengine ni ya kusesitiza tu kwa sababu msikilizaji tayari ana jibu. Maswali hayo yamechochea hisia za wahusika kwa namna tofauti.

3.4.2. Tashihisi / Uhuishaji.

Wamitila (2003) anasema kuwa tashihisi ni tamathali ambayo vitu visivyokuwa na uhai huonyeshwa kwa namna iliyo sawa na binadamu na kuweza kufikiri au kuhisi namna afanyavyo binadamu. Uhai hutwiwa kwenye vitu hivyo vilivyokuwa vitulivu na kuonekana kuwa na mwendo na kufanya vitendo mbalimbali. Kwa njia hii, usanii unaimarika. Mohamad (1995) anasema kuwa tamathali hii hufanya hisia za mlengwa kugusika na kazi aliyoiwasilisha msanii.

Tashihisi hutia nguvu katika kuzigusa hisia za msomaji au msikilizaji, kutia nguvu na harakati kwa vitu vya kawaida na vitulivu na kuonyesha kuwa na harakati mbalimbali. Inaweka maana ya fasihi wazi na kuimarisha usanii katika kazi hiyo. Ifuatayo ni mifano ya tashihisi zilizotumika katika *Utenzi wa Katirifu*;

Mtunzi anasema kuwa moyo wa Myahudi ulirudi. Moyo umepewa sifa za kuhisi na kutenda vitendo sawa na binadamu kiumbe aliye na uhai anaye na uwezo wa kwenda na kurudi (ubeti 14).

Pili mtunzi anasema kuwa Amri aliushinda moyo wake. Ina maana kuwa moyo una nguvu za kushindana na Amri. Katika mashindano hayo moyo unashinda. Moyo umepewa nguvu na hisi sawa na za mnyama au binadamu. Hayo ni matumizi ya tashihisi au uhaishaji.

Omar anaposafiri, safari inamchukua masaa matatu. Mtunzi anasema kuwa jua lilipofika (ubeti 139). Jua lilipewa sifa za kuja kama vile viumbe wafanyavyo.

Mtunzi anaelezea kuhusu nyoyo za Ali na wafuasi walipokuwa wakijiandaa kwa vita. Anasema kuwa *nyoyo zilitisha, zikalia na kutetemeka kwa ujasiri* (ubeti 169). Mtume Muhammad (S.A.W) anapozungumza nao, anawaambia walishe wanyama na

kujiandaa kwa vita. Kwa kawaida nyoyo haziwezi kulia, kutisha wala kutetemeka. Hii ni sifa ya uhaishaji iliyotumika.

Katirifu anaposikia kuhusu maandalizi yaliyofanywa na adui zake, moyo wake unashikwa na hasira (ubeti 186). Mambo yaliyokuwa yakitayarishwa yalimtia hasira. Moyo umepewa sifa kama vile binadamu anayeweza kushikwa na hasira.

Vita vinapoendelea mtunzi anasema kuwa *mikuki ilikuwa inaruka mbele na nyuma* (ubeti 324). Mikuki haiwezi kuruka ila ni ndege na viumbe walio na uhai huwa na uwezo wa kuruka. Hayo ni matumizi ya mbinu ya uhaishaji katika *Utenzi wa Katirifu*.

3.4.3 Tashibihi.

Wamitila (2003) anasema kuwa hii ni tamathali ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa namna iliyo wazi kwa kutumia viunganishi kama vile: ja, mfano wa, mithili ya na kama. Nao Kimoli na King'eli (2001) wanasema kuwa ni kulinganisha vitu vinavyokuwa na sifa zinazokaribiana kisura au kitabia. Mbinu hii pia huitwa tashibihi au mshabaha. Mohamed (1995) anasema kuwa tashibihi inapotumika maana, dhana, au hali fulani huwekwa wazi katika matumizi ya tamathali ya tashibihi.

Katika utafiti huu, tumeihakiki mifano ya tashibihi zilizotumika katika *Utenzi wa Katirifu* kwa kutoa mifano kutoka kwenye utenzi wenyewe kisha maana zinazoibushwa na tashibihi hiyo.

Mtunzi anaitumia tashibihi kuelezea namna umati ulivyokuwa baada ya Bilali kutangaza vita. Anasema kuwa *umati ulimea kama mmea* (ubeti 100). Mtunzi anasema kuwa walitaka kuenda vitani ili kupata wokovu. Jambo hili linamaanisha kuwa umati uliendelea kuwa mkubwa.

Mtunzi ameitumia tashibihi *umati ulikuwa ukivuma kama upepo* (ubeti 106). Hiini tashibihi inayoelezea kuhusu watu waliofika. Wanaume mia saba walifika kwa tangazo hilo la Bilali. Hiyo inaonyesha kuwa watu waliofika walikuwa wengi na waliingia kwa kishindo.

Omar anapoondoka kuenda Isibani kuona matayarisho ya maadui, safari ya siku tatu ilimchukua masaa matatu kana kwamba alikuwa ndege. Mtunzi anaitumia tashibihi akauka *kinga nyuni, kama aliye ba'iri* (ubeti 37). Mtunzi anamlinganisha na nyuni na kisha ngamia. Ameyarudia hayo katika ubeti 144 anaposema kuwa aliruka kama nyuni.

Mtume Muhammad (S.A.W) anaelezea namna mwanamume jasiri huonekana. Anasema *kuwashujaa hunyenyekea, kama ncha kali ya hanjari* (ubeti 158). Anamlinganisha Zuberi na ncha kali ya kisu. Inaonyesha kuwa alikuwa mpole lakini mkali vitani.

Nyoyo za wafuasi zinaelezewakukasirika *kama t'ange kuu nari* (ubeti 169). Hasira zinalinganishwa na moto uliotawala nyoyo za wafuasi wa Mtume Muhammad (S.A.W). Hasira hizo zinalinganishwa na moto ulioenea katika msitu. Jambo hili linaonyesha kuwa hasira hiyo ilikuwa vigumu kuizima namna inavyokuwa vigumu kuzima moto katika msitu.

Katirifu anarejea kumwelezea Hasina kuwa alikuwa ameshindwa vitani. Mwanzoni Hasina anataka kumkimbia. Mbio hizo zinalinganishwa na ndege (ubeti 379). Anamhimiza kurejea vitani na huko anauliwa.

Mfalme Jeusizo anasema kuwa *umati ulikuwa umefika kama watunga ghanamu au watunga ba'iri*. Makundi yaliyokuwa yakifika yanalinganishwa na wachungaji au makundi ya ngamia. Wachungaji hawa wanaonyeshwa kuwa wengi kwa namna

walivyofika. Hata hivyo, hakukuwa na wapiganaji kati yao. Wingi wao umelinganishwa na wachungaji wa wanyama au makundi ya ngamia.

Uadui kati ya wafuasi wa Mtume Muhammad (S.A.W) na Warumu na Wahabeshi unalinganishwa na pamba na moto. Mtunzi anasema kuwa *uhusiano wao ni kama wa pamba na nari* (ubeti 180). Kauli hiyo inaonyesha kuwa hawakuwa wanasikizana.

Katirifu anapowaona maadui wakija kwa safu, yeye pia aliamua kuyapanga makundi yake katika safu. Mtunzi anasemamakundi yalijipanga *kama kutanda kwa Hariri* (ubeti 193). Mpangilio huo unalinganishwa na mpangilio wa hariri inapopangwa na kufumwa.

Wingi wa makafiri unalinganishwa na uchache wa wafuasi wa Mtume Muhammad (S.A.W). Mtunzi anasema *walikuwa kama kutupa jiwe ndani ya bahari* (ubeti 197). Hiyo inaonyesha kuwa athari yao haingeonekana kwa sababu ya uchache wao. Waislamu walikuwa wachache ikilinganishwa na idadi ya makafiri. Athari yao ilikuwa ndogo sana katika vita hivi.

Mtume Muhammad (S.A.W) anapowaahidi wafuasi kuwa hawataingia motoni siku ya kiyama, wanashikwa na hamu kuu ya kuendelea kupigana. Anasema kuwa watu *walifuulia zita kama moto mwenye nyota* (ubeti 205). Huo ni moto ambao ulikuwa na kiu ya kuchoma. Ni mlinganisho wa moja kwa moja uliotumika.

Mtunzi anaelezea kuhusu hali halisi iliyokuwa vitani. Anasema kuwa *watu walipigana kweli kana kwamba mbingu ilikuwa inaanguka* (ubeti 198). Hii inaonyesha kuwa vita hivyo vilikuwa vikali mno ambavyo vingefanya dunia kuanguka.

Hawani na Khalid wanapopigana, Khalid anaonekana kushindwa. Mikdadianawasili kama ulimi wa nari (ubeti 215). Tashibihi hiyo imetumika kuonyesha kuwa Mikdadi alikuwa mkali kwa kuwa alimzidi Hawani. Baadaye, Hawani anaonyeshwa akilia.

Ali alipofika vitani, kila mtu anaanza kukimbia kwa kumwogopa. Mtunzi anasema walikuwa wakichomwa kama samaki ambao walikuwa wamevuliwa(ubeti 327) na wengine kukimbia na kuvunja vichwa vyao kama baidha tuyuri. Mtunzi anamaanisha kuwa walivunjwa vichwa vyao kama mayai ya ndege. Maelezo hayo ya kulinganisha yanaonyesha namna Ali alivyokuwa mkali vitani.

Kidari naye anashikwa na aibu anaposhikwa na Ali. Aibu aliyokuwa nayo ilimfanya kujiua. Mtunzi anasema *akayitia motoni kama p'andi uyalini*. Alijitia motoni kama panzi kwa sababu alitaka kujiondoa kutoka kwenye aibu.

3.4.4 Chuku.

Chuku ni maelezo yaliyotiliwa chumvi. Jambo la kawaida huajabishwa likaonyeshwa kuwa kubwa kupita kiasi au kudunishwa kupita kiwango. Kulingana na Kuhenga (1977) lengo kuu la kutumia chuku ni kutilia mkazo kitu au jambo au hata hali za mtu fulani. Maelezo mengi katika *Utenzi wa Katirifu* yametiliwa chumvi.

Katirifu anapofika kwa Hasina anaambiwa kwamba mwanzo amkamate Ali na Mtume Muhammad (S.A.W) ndipo apate kumwoa. Anasema kuwa anaenda kukusanya kaumu kwenye miji yote ya Warumu ambao wangukuwa wengi kushinda nyota. Hayo ni maelezo yaliyotiliwa chumvi kwa kuwa wingi wa binadamu hawezi kushinda wingi wa nyota (ubeti 47).

Safari ya kwenda Isibani kwa kawaida ilichukua siku kumi na moja. Wafuasi walitembea na kufikia siku ya nane walikuwa wamekaribia Isibani. Hii ni kwa

sababu ya hamu kuu waliyokuwa nayo ya kumpigania Mtume Muhammad (S.A.W) vitani. Mtunzi ametumia mbinu ya chuku katika kuelezea hamu hiyo (ubeti 127-128).

Omar anapoondoka kwenda Isibani, anatoka kwa nguvu nayo safari ya siku tatu milimani na kwenye misitu inamchukua masaa matatu (ubeti 138). Ni maelezo yaliyoongezewa chumvi kwa kuwa siku tatu ni nyingi ikilinganishwa na masaa matatu.

Omar anapoingia anatifua vumbi mpaka waliokuwepo wakafikiri ni Ali (Sheikh). Mtunzi anasema vumbi lilifanya jua kupotea na watu kukosa kuona na kupumua. Baadaye waligundua kuwa alikuwa Omar wala si Ali.

Watu wanapoomba, mtunzi anasema kuwa machozi ya Mtume Muhammad (S.A.W) yaliwaliza malaika na kuifanya mbingu kutetemeka, milima na mabonde vilevile. Machozi tu hayawezi kufanya mambo kama hayo kufanyika. Ni maelezo yaliyotiliwa chumvi (ubeti 306).

Walipoinuka kutoka kwa maombi upepo mkali ulitokea ambao ungeweza kumbeba ngamia. Kwa kawaida ngamia ni mzito hawezi kubebwa na upepo. Ni maelezo kuonyesha kuwa upepo huo ulikuwa mkali kabisa (ubeti 308).

Ali anapokuwa vitani anafanya mambo ya ajabu yasiyoweza kufanywa na binadamu wa kawaida. Aliishika Dhu L'Fikar (upanga) na kuwauma watu kwa meno hasa wale waliojaribu kumshika. Ana nguvu zilizopita kiasi hivi kwamba angemwangalia mtu na mtu huyo kufa papo hapo macho yake yakiwa wazi (ubeti 319-332). Anaonyeshwa kuwa mtu mwenye nguvu nyingi.

Ali anapokutana na Kidari vitani, anamzomea hadi Kidari anashikwa na aibu. Kwa sababu ya aibu hiyo, anaamua papo hapo kujirusha motoni. Si jambo la kawaida mtu

kushikwa tu na aibu hadi anajirusha motoni. Ni maelezo tu ya mtunzi ya kutilia chumvi.

Kwa mkuki mmoja tu Kidari na wapiganaji wenzake wanauawa. Ali alishikwa na hasira na hakutaka kusikiliza tena. Hiyo inamfanya Katirifu kurejea kwa Hasina anayemhimiza kurejea vitani (ubeti 308-309). Mkuki mmoja tu kurushwa hauwezi kuwaua watu wengi kwa pamoja labda mtu mmoja tu. Hayo ni matumizi ya chuku.

Kwa pigo moja tu kichwani, Sheikh Ali anampasua Katirifu kwa vipande viwili. Anapokufa shimo linafunguka kimiujiza naye akazama na huo ukawa ndio mwisho wake (ubeti 396). Pigo moja tu la kawaida haliwezi kumpasua mtu kwa vipande viwili. Hili linamfanya Hujam kujiondoa vitani na makundi yote aliyoyaongoza kumfuata.

3.4.5 Sitiari.

Sitiari ni tamathali inayotumia ulinganishi wa moja kwa moja. Maneno ya ulinganishi hayatumiki. Ulinganishi unaofanywa unafanya sifa za kitu kimoja kutumika kuelezea kitu kingine bila kilinganishi. Wamitila (2008) anasema kuwa kilinganishi, kilinganishwa na sifa za ulinganishi huangaliwa kabla ya kuunda sitiari.

Neno Haidari limetumiwa katika utenzi huu kurejelea simba ila si simba mnyama. Limetumiwa kumrejelea Ali kwa sababu ya ukali na nguvu zake. Ukali na nguvu hizo ni kama ule wa simba. Yeye ndiye shujaa anayemaliza vita katika utenzi huu. Sifa anazopewa zimefananishwa moja kwa moja na zile za simba mnyama. Jina lingine linalotumiwa kumrejelea Ali ni kama vile mvunja miji (ubeti 75).

Majina ya kisitiari pia yametumiwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W). Badala ya kumwita kwa jina mtunzi anatumia muungamu, muongofu, mtumwa wa mungu,

mwaminifu n.k. Majina hayo yanabainisha sifa alizo nazo Mtume Muhammad (S.A.W) na majukumu aliyokuwa nayo katika jamii hii.

Mtunzi anasema kuwa Sheikh Ali anaenda kushenga nyama badani, dhiri'amu na chui. Dhiri'amu ni simba na namiri ni chui. Si wanyama wanaorejelewa katika kauli hii ila ni binadamu walio na ujasiri kama ule wa simba na chui. Simba na chui ni vilinganishwa vya binadamu. Sifa ya ulinganishi iliyopo ni ushujaa. Hawana woga wowote. Mhusika mwingine aliyetitwa simba ni Mikidadi (ubeti 109-110)

Mbinu ya kisitiari huwa na maana mbili. Maana iliyo wazi na ile iliyofichwa. Mbinu ya kisitiari imejikita katika kiwango cha kisemantiki kwa kuwa inamhitaji msomaji kufikiria ili kupata maana iliyofichika ya maneno fulani. Mbinu huu hukiuka semantiki kwa kuwa itamhitaji msomaji au msikilizaji kufikiria ili kupata maana iliyofichika.

3.5 Uhuru wa Kishairi.

Kulingana na Abedi (1954) mashairi yanapoandikwa hufuata kanuni za utunzi wa mashairi. Kanuni hizo ni kama vile: inkisari, mazida, lahaja na matumizi ya msamiati wa zamani.

3.5.1 Inkisari.

Inkisari mbinu inayotumiwa na watunzi wa fasihi hasa mashairi ya kufupisha maneno. Mengi ya maneno yaliyotumika katika *Utenzi wa Katirifu* yamefupishwa ili kutosheleza idadi ya mizani katika beti husika. Tumeiteua mifano michache tu kuthibitisha hayo nayo ni ifuatayo:

Wajawe-waja wake (ubeti wa 4, mshororo wa 1)

Nuruye-nuru yake (ubeti wa 9, mshororo wa 1)

Moyowe-moyo wake (ubeti wa 17, mshororo wa 3)

Akiliye-akili yake (ubeti wa 27, mshororo wa 1)

Jinale-jina lake (ubeti wa 29, mshororo wa 1)

Minaye-mimi na yeye (ubeti wa 37, mshororo wa 4)

3.6 Lahaja.

Lahaja ni vijilugha vidogo vidogo vya lugha moja ambavyo hubainika kijamii au kijiografia. Lahaja hutofautiana katika matamshi, miundo ya sarufi na msamiati uliotumika. Lahaja hutofautishwa kulingana na vipengele vifuatavyo: vipengele vya sera, maoni ya wasemaji wa lugha husika, jamii na maeneo.

Baadhi ya maneno yaliyotumika katika *Utenzi wa Katirifu* ya lahaja ya Kiamu ni yafuatayo:

Nti-nchi

Kaata-kaacha

Mtunga-Mchungu

Nyani-nani

Yinale-jinale

Ayapo-ajapo

3.7 Matumizi ya Kiswahili cha kale au zamani.

Baadhi ya maneno yaliyotumika ni maneno ya Kiswahili cha kale mno. Hiki ni Kiswahili cha lahaja ya Kingozi kwa kuwa ndicho kilikuwa Kiswahili kilichokuwa kimeimarika wakati huo. Lahaja ya Kingozi ilitumiwa kabla ya kukua na kuimarika kwa lugha ya Kiswahili. Mfano wa neno lililotumika ni upendakyo badala ya upendacho katika ubeti wa 23 mshororo wa 3.

Katika lahaja na matumizi ya maneno ya zamani, kiwango cha fonolojia huangaliwa na jambo hilo kwa kiwango kikubwa huathiri semantiki.

3.8 Hitimisho.

Katika sura ya tatu, tumejadili mbinu za lugha zilizotumika katika *Utenzi wa Katirifu*. Mbinu hizi zimetumika kwa ustadi mkubwa ili kuwasilisha maudhui ya mwandishi huyu. Zimetumiwa kuwasilisha maudhui mbalimbali na pia kuathiri hisia za msomaji kwa namna moja au nyingine. Hisia kama vile chuki, udhalimu, huruma na hata pongezi kutolewa kwa washindi katika vita hivyo. Mbinu zilizotumiwa ni taswira na dayalojia na tamathali nyingine za usemi kama vile tashihisi, maswali ya balagha, tashibihi, chuku na sitiari. Mbinu hizi zimetumiwa kuibua maana, hisia za wahusika, kuhuisha na pia kuirembesha kazi hii.

Katika sura hii tumejadili matumizi ya mbinu za kishairi ikiwemo inkisari. Lahaja na matumizi ya Kiswahili cha zamani pia zimehakikiwa. Kuhusu muundo na usimulizi, kazi hii imewasilishwa kupitia kwa mbinu rejeshi. Kazi hii ina mwanzo, kati na mwisho. Katika mwanzo kuna mgogoro wa pande mbili unaomalizika kwa suluhu kupatikana.

SURA YA NNE

MANDHARI NA USIMULIZI.

4.1 Utangulizi.

Kitendo chochote kile katika fasihi hutendeka au hufanyika katika sehemu fulani iliyoteuliwa kwa ajili ya shughuli hiyo. Vitendo hivyo pia hufanyika wakati maalum. Dhana mandhari huelezea ni wapi na ni lini tendo hilo lilipofanyika. Wamitila (2003) anaelezea mandhari kuwa wakati au mahali katika tamthilia au hadithi palipotokea utendaji fulani. Pia yanaweza kuwa mazingira yanayomzunguka mwandishi. Mazingira haya yanaweza kuwa ya kijamii au kielimu.

Njogu na Chimera (1999) wanafafanua dhana mandhari kuwa ni mahali maalum au mnamotendeka matukio fulani katika kazi ya fasihi. Inaweza pia kuchukuliwa kuwa mahali wanamokaa wahusika na yote yanayowahusu kama vile uchumi, siasa, tabaka au hata maswala ya kijamii. Mandhari kwa kiwango kikubwa hurejelea mila, desturi, itikadi na elimu za jamii inayohusika. Pia hutegemea muktadha wa kazi husika ya fasihi. Mandhari huchangia pakubwa katika kukuza tabia nahali za wahusika mbalimbali na maudhui wanayoyaendeleza katika kazi fulani ya kifasihi. Sifa na tabia za mhusika huweza kuchochewa na mandhari na pia kuelezewa kupitia kwa mandhari.

Mandhari hubadili sifa na tabia za wahusika katika fasihi. Maudhui ya mtunzi pia hukuzwa kupitia kwa mandhari. Aghalabu kila tendo katika fasihi hutegemea pakubwa mandhari na wahusika katika utendaji. Hivyo, sifa na tabia za wahusika huathirika pakubwa na mazingira ambamo mhusika hujikuta.

Matendo huchochewa na mandhari. Mazingira huathiri kwa kiwango kikubwa tabia za wahusika mbalimbali. Hii ni kwa kazi zilizoandikwa kwa kuzingatia misingi ya

kihalisia. Mandhari ya kazi za aina hii huweza kutambulika kwa njia iliyo wazi na ya moja kwa moja katika kazi iliyo na muundo sahili. Kazi yenye muundo sahili hupendwa na wasomaji kwa kuwa wasomaji wengi hupenda mandhari yanayotambulika kwa urahisi. Hata hivyo, baadhi ya kazi za fasihi huwa zimeundwa katika misingi ya kiuhalisiajabu na hivyo inakuwa vigumu kwa msomaji kutambua mandhari lakini katika kazi zilizotungwa katika misingi ya uhalisia inakuwa ni rahisi mno kwa msomaji kutambua mandhari.

Mandhari hutoa mchango muhimu katika kazi yoyote ile ya fasihi. Umuhimu huo hutegemea dhamira ya mtunzi wa kazi husika. Kupitia kwa mandhari msomaji au msikilizaji hupata uelewa kuhusu wahusika waliotumiwa kihisia, kimaumbile, kitabia na hata kiimani.

Kuna aina mbili za mandhari zilizotumiwa katika *Utenzi wa Katirifu*. Kuna mandhari halisi kama vile nyumbani, msituni au hata pangoni. Wamitila (2002) anasema kuwa matukio ya kihistoria yanaweza kuwa mandhari ya vipindi maalum vya historia. Vipindi hivyo huweza kuchukuliwa kuwa mandhari. Kwa mfano vipindi vya vita vya kwanza vya dunia na vile vya pili. Pili, kuna mandhari yasiyo halisi au ya kinjozi. Hujikita katika sehemu za kufikirika tu. Ni mambo yasiyowezekana katika ulimwengu wa kawaida. Katika *Utenzi wa Katirifu*, kuna mandhari ya kinjozi na pia halisi.

4.2 Mandhari.

4.2.1 Mandhari halisi.

Mandhari halisi pia huitwa mandhari ya kijiografia. Katika aina hii ya mandhari, mtunzi huweza kuelezea mazingira kana kwamba msomaji anafahamu mazingira hayo na kuwaona wahusika hao. Hata hivyo, wahusika ni wa kubuniwa na kazi

enyewe ni ya kibunifu. Jukumu kuu ni kumfanya msomaji kuamini kuwa matukio hayo yanaweza kuwepo, kufanyika na kukubalika katika mazingira halisi.

Mtunzi anaanza utenzi huu kwa kukusanya vifaa ambavyo angetumia katika kutunga kazi yake. Anasema kuwa anataka kusimulia yale yaliyotendeka katika nchi ya Shamu. Anaendelea kusema kuwa kila mtu anaifahamu hadithi hii kwa kuwa haya ni matukio ya kweli. Tukio analolisimulia ni la kihistoria (ubeti 12-13). Haya ni mandhari halisi kwa kuwa ni tukio lililowahi kufanyika katika historia ya maisha ya watu wa Shamu.

Pili, kuna mandhari ya jangwani. Hii ni sehamu anapokaa Hasina. Hasina amerithi mali aliyokuwa nayo babake. Jumba analokaa ni la kuvutia na ni vigumu kupata majumba ya aina hiyo jangwani. Kupitia mandhari ya jumba hili na jangwa, tunapata kuelewa zaidi kuhusu tabia ya Hasina na pia babake. Mtunzi amemwelezea kuwa alikuwa mtu mwovu na Hasina pia alifuata tabia hizo. Jambo hili lina maana kuwa Hasina alikuwa mwovu kama babake.

Hasina anamtaka Katirifu aende akaivamie Arabia. Anamtaka Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali wauliwe kwa kuwa anasema kuwa wake zao na wana wao wasiwaone tena. Kwa kutaja Arabia, ni wazi kuwa hii ni sehemu inayopatikana na kujulikana ulimwenguni. Maeneo halisi alipofaa kukamatwa Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali panajulikana. Haya ni mandhari halisi.

Amri anasimuliwa kisa cha Katirifu kwenda kumkamata Mtume Muhammad (S.A.W). Anakasirika na kumwambia mchungaji aache kusimulia. Kwa hasira, anaondoka na kuenda Medina. Medina ni mandhari halisi. Mtunzi anaendelea kuelezea kuwa ni sehemu iliyokuwa na ua uliokuwa kwa pamoja na hakuna nafasi

hata kidogo iliyoachwa. Kuna mandhari ya msikiti na Mtume Muhammad (S.A.W) alikuwa ameketi na wafuasi wake.

Mandhari na maelezo yanayotolewa kuhusu alipokuwa Mtume Muhammad (S.A.W) na wafuasi wake yamesaidia mno kumkuza Mtume Muhammad (S.A.W) kama mhusika na pia Amri. Sifa za uhalisiajabu kama vile uso wake kung'ara inaonyesha kuwa alikuwa na nguvu na uwezo uliopiku binadamu wa kawaida. Pia, anaonyeshwa kuwa mwenye mapenzi kwa kuwa anawakubali kwa haraka wale wanaoasi dini zao na kuingia katika Uislamu.

Amri anapokuja njiani anakutana na mchungaji. Kupitia mbinu rejeshi mandhari ya malishoni yanaonyeshwa kwa kuwa Mwarabu alikuwa mchungaji. Hata kama ni jangwa kuna mifugo wanaolindwa na mchungaji huyu.

Amri anapokuwa safarini anakutana na mtu. Mandhari ni jangwani. Huko kumejengwa jumba zuri ila limezingirwa na watu wa tabaka la chini. Lilikuwa jumba kubwa na shamba vile vile. Ni mandhari yanayoweza kuaminika kwa kuwa wengi huishi katika sehemu zilizozingirwa na wanyonge au maskini wa tabaka la chini. Ni wanyonge watakaotumiwa na matajiri ili kuendelea maishani.

Pili, kuna mandhari ya vita (ubeti 125-127). Wafuasi wa Mtume Muhammad (S.A.W) wanaondoka na kuenda vitani wakiwa wamemzingira. Vitani damu nyingi inamwagika na watu wengi kufa ila kuna yasiyowezekana kama watu kupigana na wengine wakiwazika wafu. Hilo haliwezekani katika mazingira ambamo kuna vita.

Malaika Jibrili anashuka kuleta ujumbe kuwa Mtume Muhammad (S.A.W) ajitayarishe kwa vita. Papo hapo, Bilal anaitwa ili atangaze vita. Bilal anafika na kutangaza vita. Mandhari ya utakatifu na viumbe takatifu yanaonyeshwa hapa.

Baada ya vita kutangazwa, mandhari ya vita yanafuatia. Kuna makundi mawili yanayojitayarisha. Kundi la Mtume Muhammad (S.A.W) na lile la Katirifu. Katika kundi linaloongozwa na Mtume Muhammad (S.A.W), kikundi cha kwanza kinaongozwa na Za'id bin Katibu Said, kisha kikundi cha pili kilichokuwa na wanaume mia mbili walioteuliwa na waliojulikana. Baadaye, kuna kundi la wanaume 700 walioteuliwa na waliokuwa na viongozi wanne. Mbele yao kulikuwa na jiwe na kulifikia tu wakagawanyika. Mandhari haya yanayoonyesha matayarisho ya vita yanawakuza wahusika kama vila Mikdad, Zahr bin Ma'ad, Omar bin Hatab na Khalid bin-Walid. Sifa zao za ushujaa na hasa ile ya kujitolea kuongoza katika vita zinabainika katika sehemu hii.

Majeshi yote yanaonyeshwa kuwa yalikuwa yamejitolea kuingia vitani. Katika kuongoza makundi haya Zobeir bin Awam anapewa jukumu la kuongoza makundi haya. Anapewa bango na Mtume Muhammad (S.A.W). Bango hilo Mtume Muhammad (S.A.W) alikuwa amelirithi kutoka kwa babuye aliyekuwa Mmaka. Omar na Mikdad wanapewa jukumu la kutembea mbele ya makundi haya na mabango waliyopewa kuyabeba.

Mtunzi ametuchorea picha ya wapiganaji wakiwa katika safu kuelekea Isibani kulikokuwa na vita. Safari yao ni ya usiku na mchana. Wamemzingira Mtume Muhammad (S.A.W). Safari ya siku kumi na moja inawachukua siku nane. Njiani Mtume Muhammad (S.A.W) anamtuma Umar bin Umayya aende mpaka Isbani na kumuahidi kuwa atamwepusha na adhabu ya moto. Safari ya siku tatu inamchukua masaa matatu tu. Jambo hili linamkuza mhusika huyu na kumwonyesha kuwa mwenye mapenzi ya dhati kwa dini yake.

Sehemu ya vita vyenyewe pia inaonyeshwa. Mtunzi anasema kuwa visu vilimetameta. Mabango ya makafiri yalikuwa mia tano. Hirizi moja ilikuwa na watu 600,000 na nyingine watu 1,300,000. Ujasiri wa mhusika Umar bin Umayya unaonyeshwa hapo. Kati ya watu wote yeye ndiye aliyejitolea kwenda kuutazama uwanja wa vita na kuleta ripoti.

Ali anaota ndoto ya ajabu akiwa katika mazingira yake halisi. Hata hivyo, anachoota kinasadfa kuwa ndicho kilichokuwa kikiendelea katika hali halisi. Anapoamka kutoka usingizini anaamua kuwa ni sharti aende kumsaidia Mtume Mohammad (S.A.W).

Vitani kuna mapigano makali. Kila kundi linakusanya majeshi yake katika kila upande. Kwa kila ahadi anayoitoa Mtume Muhammad (S.A.W) mapigano yanazidi. Mtunzi anaelezea kuwa hakuna aliyeweza kumwokoa mwingine. Damu iliteremka kama iliyo kwenye mto na idadi ya waliouliwa ni mia saba. Wanapokelewa na malaika wanapofika mbinguni.

4.2.2 Mandhari ya kinjozi.

Mandhari ya kinjozi ni mandhari yasiyoweza kuhusishwa na uhalisi katika *Utenzi wa Katirifu*. Wahusika hutoka katika ulimwengu halisi na kuenda katika ulimwengu wa kinjozi na kisha huweza kurejea tena katika ulimwengu halisi. Mandhari yafuatayo ya kinjozi yameshughulikiwa katika *Utenzi wa Katirifu*.

Baadhi ya sehemu zilizotajwa katika utenzi huu hazina uhalisi katika ulimwengu wa kawaida. Kwa mfano, kule vitani, Ali anaonyeshwa kuwa na nguvu kupita kiasi. Mtunzi anasema kuwa mkono wake ungeshikilia kama bawaba na hata kuwaumiza wengine vitani kwa meno tu. Angeuchukua hata uhai wa mtu kwa kumtazama tu.

4.3 Usimulizi.

Katika fasihi simulizi, msimulizi huwa mbele ya hadhira yake wakati anaposimulia. Hili lina maana kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya msimulizi na wasikilizaji. Hadhira inaweza kushirikishwa katika usimulizi wa aina hii hasa msimulizi anapotumia nyimbo katika kuwasilisha matukio yake. Katika usimulizi wa fasihi simulizi, hisia za msimulizi pamoja na zile za hadhira huweza kuonekana moja kwa moja. Huzuni, furaha, hasira, kushangaa na hata kuitikia huonekana moja kwa moja. Zinaweza kutokea katika upande wa msikilizaji au hata kwa upande wa msimulizi.

Baadaye, kulivumbuliwa maandishi. Fasihi simulizi na yote yahusianayo na fasihi simulizi yakatoweka. Yaliyotendeka katika fasihi andishi yakawa kinyume cha fasihi simulizi. Ule ushirikisho wa moja kwa moja na hadhira ukatoweka. Hadhira haikupata kushirikishwa tena katika usimulizi. Hisia za msikilizaji na msimulizi hazikutambuliwa tena kwa kuwa msikilizaji sasa alikuwa akisoma tu.

Usimulizi umefafanuliwa na wataalam tofauti kwa namna tofauti. Attenbernd na Lewis (1963) wanasema kuwa usimulizi ni mkabala wa kuiwezesha hadhira kuyatazama yatendekayo na kusikia yanayozungumzwa katika fasihi. Naye Mlacha (1991) anasema kuwa usimulizi ni uhusiano kati ya msimulizi na anachosema. Nafasi katika uwasilishaji husaidia katika kuelewa usimulizi wa mtunzi wa fasihi husika.

Katika mwingiliano huo, mwelekezi wa hadithi huweza kutambuliwa na pia mtazamo na uhusiano na matukio katika hadithi husika. Uhusika wake pia huweza kuangaliwa kwa mkabala wa mhusika. Katika hali hii, kazi husika inafaa kuwa na mtazamo unaoweza kuaminika kuhusu matukio. Hata hivyo kuna mitazamo mingine isiyoweza kuaminika hasa kuhusiana na kazi zilizotungwa katika msingi wa kiuhalisiajabu.

Wales (1990) anaeleza usimulizi kuwa ni mchakato wa mawasiliano unaotokea kati ya mtunzi na msomaji au msikilizaji wake. Wamitila (2003) anaifafanua dhana usimulizi kuwa ni namna ya kuelezea matukio katika hadithi. Ni mbinu inayotumiwa na mtunzi ili kuwasilisha ujumbe kwa msikilizaji au msomaji wa kazi ya kifasihi. Njogu na Chimera (1999) wanasema kuwa usimulizi ni sauti inayotumika na mtunzi katika kuwasilisha matukio yaliyoko katika hadithi.

Mtunzi wa *Utenzi wa Katirifu* ametumia fani ya kishairi katika kuwasilisha kazi yake. Tamthilia hutumia mbinu ya kidrama nazo riwaya hutumia mbinu ya kisimulizi. Ni sharti usimulizi utumike katika fasihi kwa kuwa kupitia usimulizi ndipo msomaji au msikilizaji hupata habari au ujumbe uliokusudiwa.

Usimulizi unaweza kuwa wa moja kwa moja au usiwe. Usimulizi usiokuwa wa moja kwa moja huwa changamano. Hii hutokea mbinu rejeshi inapotumiwa katika kazi ya fasihi. Tamthilia huwa na mazungumzo ya moja kwa moja kwa hivyo huenda usimulizi usitumike. Kazi nyingine kama vile riwaya sharti zitumie usimulizi. Nafsi pia huchangia katika usimulizi. Kuna nafsi ya kwanza, pili na tatu. Nafsi hizi hutumika kulingana na msanii wa fasihi husika.

Hata ingawa usimulizi hutumiwa mno katika riwaya, umetumika katika *Utenzi wa Katirifu* kwa kuwa ni masimulizi ya mambo yaliyokwisha kutendeka hapo awali. Usimulizi uliotumika katika *Utenzi wa Katirifu* ni wa moja kwa moja kwa kuwa kila kinachoelezewa kinaeleweka moja kwa moja. Kuna aina nne za usimulizi zilizotumika katika *Utenzi wa Katirifu*.

4.3.2 Mbinu za usimulizi.

Kuna mbinu nyingi zinazotumiwa katika usimulizi. Mbinu iliyoteuliwa hutegemea kabisa mada husika. Kila mada huibua hisia tofauti. Ikiwa ni mada inayohusiana na

vita basi hisia zitakazokuwepo ni za huzuni na iwapo mada itahusu harusi basi hisia za furaha zitatalaki. Kazi nyingine zitakuwa za kutahadharisha au kufahamisha kuhusu kinachosimuliwa. Kila mbinu inayoteuliwa hutegemea pakubwa kinachokusudiwa.

4.3.2.1 Usimulizi wa nafsi ya kwanza

Katika usimulizi wa aina hii, msimulizi huchukuliwa kuwa mmoja kati ya wahusika katika kusimulia hadithi yote. Mohamed (1995) anasema kuwa usimulizi wa nafsi ya kwanza huwa si mbinu rahisi kwa mwandishi kwa kuwa viwakilishi vya nafsi havifai kutumika kwa wingi bali umoja tu. Hivyo, inamhitaji kuwa makini mno asije akachanganya viambishi hivyo. Hata hivyo, usimulizi wa nafsi ya kwanza haujatumika sana katika Kiswahili.

Baadhi ya sifa zinazoutambulisha usimulizi wa aina hii ni mwandishi kubanwa. Si mambo mengi anayoweza kuyasema au kuyaweka wazi. Ni mtu mmoja tu anayetegemewa hivyo habari wanazozipata wasomaji wa kazi ya aina hii huwa zimebanwa. Ikiwa mazungumzo kati ya mhusika na mwingine yatafanyika au mbinu nyingine kama vile matumizi ya barua kutumika, wasomaji wataweza kupata mtazamo mwingine ambao hajatajwa na msimulizi wa aina hii.

Mawazo ya msimulizi wa nafsi ya kwanza na yale ya mwandishi wa kazi huweza kuangaliwa kwa namna tofauti kwa kuwa yanachukua mitazamo tofauti. Hata hivyo, mtazamo wa kazi husika huangaliwa kupitia kwa mhusika maalum. Mtazamo huo hueleweka kwa aina fulani ya mhusika tu.

Matukio katika usimulizi wa aina hii huonekana kana kwamba ni matukio ya maisha ya kila siku na kuchukuliwa kuwa ni mambo ya kawaida. Sifa ya mwisho ni kuwa

msimulizi huwa na uwezo wa kuficha mambo hadi pale yanapohitajika kutolewa kwa hadhira au msomaji wa kazi husika.

4.3.2.2 Usimulizi ngazi.

Wamitila (2003) anafafanua usimulizi ngazi kuwani aina ya usimulizi ambapo kuna vijihadithi vidogo vidogo ndani ya hadithi kuu. Hadithi kuu ni vita vya Badri. Ni hadithi inayomhusisha Katirifu, Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali. Katirifu anataka kuwaua Ali na Mtume Muhammad (S.A.W) kwa kuwa anataka kumwoa Hasina. Anataka kulipiza kisasi kwa niaba ya babake. Katika hadithi hii kuu, mtunzi anaziweka wazi sifa za Mtume Muhammad (S.A.W), Hasina, Katirifu na Ali. Hasina na Katirifu wanaonyeshwa kuwa watenda maovu. Ni kwa sababu ya kiu ya Katirifu kutaka kumwoa Hasina, ndipo maafu na hasara yote katika hadithi hii kutokea. Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali wanaonyeshwa kuwa ni wapenda haki na usawa katika jamii hii. Ndio maana wanakataa maovu ya babake Hasina na Hasina.

Hadithi nyingine iliyosimuliwa ni ile inayomhusu babake Hasina. Anayeisimulia ni mchungaji kwa Amri. Katika hadithi hii, mchungaji anabaini baadhi ya sifa za babake Hasina na Hasina vilevile. Anasema kuwa alipenda maovu na mwanawe akafuata tabia zile zile. Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali hawakupenda tabia hiyo na katika kuipinga, vita vinatokea. Katika vita hivyo babake Hasina anauliwa. Kifo cha babake Hasina ndio msingi mkuu wa vita katika hadithi hii.

Tatu, kuna hadithi kuhusu Amri. Asili ya Amri ni kuwa alikuwa Myahudi. Moyo wake ulibadilika na akaamua kumfuata Mtume Muhammad (S.A.W). Mtunzi anaelezea kuwa aliiacha familia yake na mali yake yote akaamua kuja kumfuata Mtume Muhammad (S.A.W). Amri ndiye anayekutana na mchungaji ambaye mtunzi anasema kuwa asili yake ilikuwa ni Mwarabu. Kutupa macho analiona jumba zuri na

kutaka kujua mmiliki wake. Wakati huo alikuwa anasimuliwa kuhusu kisa cha Katirifu. Kisa hicho kinamkasirisha hadi hataki kuendelea kukisikiliza. Anaondoka na kuenda kumwelezea Mtume Muhammad (S.A.W). Kisa hiki kinatoa mwanga kuwa kuna baadhi ya waumini wa dini wanaoasi dini zao na kuzishika dini nyingine tofauti.

Hadithi fupi inatolewa namna Kidari alivyokufa. Kidari alipoambiwa kuwa wapiganaji wengine walikuwa wameuliwa alishikwa na aibu hadi akajirusha mwenyewe motoni kama panzi. Alikatwa masikio kabla ya kuuawa. Alirejea kwa Katirifu aliyemhimiza kuwa arudi vitani. Ali anafika akiwa na hasira kuwaua Kidari pamoja na wapiganaji wenzake. Mwanzoni mtunzi ameeleza kuwa Kidari alikuwa ni mateka. Historia fupi kumhusu imetolewa kwa mfano wa kijihadithi ili wasomaji wapate kuelewa asili yake.

Matukio baada ya Katirifu kuuliwa yameelezewa kwa mfano wa hadithi. Hasina alipofika pale, alivua nguo zote akabaki uchi kisha akaanza kumshutumu na kumlaumu Katirifu kuwa mauti hayo alijisababishia mwenyewe. Badala ya kujilaumu kwa kumsukuma Katirifu kwenda kuwaua Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali, anamlaumu kwa kujisababishia kifo. Kutokana na kijihadithi hiki Hasina anaelekea kukubali kuwa Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali wana nguvu kumshinda mwanadamu yeyote yule. Anawasuta makafiri waliobaki kuwa walikuwa wajinga.

Usimulizi wa aina hii huchangia katika kukuza wahusika na vilevile maudhui. Sifa na tabia za Amri, Kidari, Mtume Mohammad (S.A.W), Ali, Katirifu, Hasina, Babake Hasina na mchungaji zimekuzwa. Maudhui ya vita, dini, haki na nafasi ya mwanamke yamebainishwa vyema kupitia kwa wahusika hawa.

4.3.2.3 Usimulizi wa nafsi ya tatu.

Huu ni usimulizi unaotumika hasa katika riwaya. Ni usimulizi unaojikita katika wahusika. Mohamed (1995) anasema kuwa ni usimulizi unaompatia mhusika nafasi ya kusimulia yanayotendeka katika hadithi. Ni kinyume na msimulizi maizi anayesimulia kila kitu. Hata, hivyo mbinu zaidi ya moja huweza kutumiwa katika kazi moja.

Matukio katika utendaji au katika fasihi ya kusomwa huelezwa kwa upana ili msikilizaji au msomaji apate kuelewa yale yanayoendelea katika kazi husika. Katika masimulizi haya ulimwengu mpya huweza kubuniwa ulioko nje ya mandhari ya hadithi iliyokuwa ikisimuliwa. Msimulizi huwa na uwezo wa kuingia katika akili ya mhusika fulani na kuelezea matukio yaliyo akilini mwa mhusika huyo. Hutembea kila mahali kwa nia ya kuelezea matukio ya mhusika fulani. Lugha inayotumiwa na msimulizi si ya moja kwa moja yaani ile ya kimazungumzo bali ni ile ya kushuhudia na kuripoti matukio katika maisha ya mhusika. Jukumu kuu la msimulizi ni kuelezea matukio ya mtu mwingine.

Wamitila (2003) anasema kuwa msimulizi huwa na siri kuhusu kila kitu. Atakuwa anawaelewa wahusika wote katika kazi husika pamoja na tabia zao na anachokusudia kukitenda. Msimulizi huhitaji kuwaelewa wahusika, mandhari na hadithi yote kwa jumla ili kuwa na ufahamu wa yote angependa kusimulia.

Usimulizi unapotumiwa katika fasihi lugha huwa ni ya kibunifu na mambo mengi huongezewa ikilinganishwa na yale ambayo mzungumzaji angeyatumia katika mazungumzo ya kitamthilia. Hivyo, fantasia hutumika ili kuyafanya matukio kubadilika kwa kiwango fulani na kuyafanya yawe ya kuvutia zaidi. Baadhi ya

mambo yasioweza kuelezeka katika hali ya kawaida, msimulizi hupewa jukumu la kuyawasilisha kwa hadhira au msomaji.

Msimulizi huwa na uhuru wa kiwango kikubwa wa kuingia popote na kuwaletea wasomaji au wasikilizaji habari kuhusu yaliyotukia. Anapoingia popote huwa kama mmoja wa wahusika katika kazi hiyo. Ingawa usimulizi kwa mara nyingi huhusishwa na riwaya, pia hudhahirika katika ushairi hasa tenzi kwa kuwa utenzi ni hadithi tu inayowasilishwa kwa mfano wa ushairi. Mifano ifuatayo ya usimulizi wa nafsi ya tatu imetumika katika *Utenzi wa Katirifu*.

Mtunzi anaanza kwa usimulizi wa nafsi hii. Msimulizi anaandaa vifaa. Anaomba apewe karatasi, wino na kalamu ili aweze kusimulia aliyoyashuhudia. Ni kana kwamba alishuhudia yaliyotendeka na sasa anataka kuwasimulia wale ambao hawakushuhudia. Anasema kuwa alisoma katika kitabu lakini namna ambavyo anasimulia matukio ni kana kwamba aliyaona. Hata hivyo mtindo anaoutumia ni wa kishairi.

Mchungaji pia anautumia usimulizi wa nafsi ya tatu. Hakumwona babake Hasina wala hakushuhudia vita kati ya babake na Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali. Namna anavyosimulia ni kana kwamba aliyashuhudia kisha kumsimulia Amri. Katika usimulizi huo anaelezea sifa za Hasina na vilevile babake. Wanadhihirishwa kuwa watu waovu. Ndipo Katirifu anapofika na kutaka posa ya uchumba. Posa hiyo ndiyo inayopelekea vita kuanza. Hata hivyo, Katirifu na Hasina hawafaulu kulipiza kisasi. Katirifu anauliwa vitani.

Amri anaposimuliwa hadithi hii ya Katirifu kutaka kumwua Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali anatoka kwa hasira mpaka Medina. Huko anamsimulia Mtume Muhammad (S.A.W) na wafuasi kuhusu alichokusudia kukifanya Katirifu.

Anautumia usimulizi wa nafsi ya tatu kusimulia haya. Ni mambo aliyoyasikia mwenyewe na kuja kusimulia moja kwa moja kwa Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali.

Katirifu anayasikiliza maneno ya Mfalme Jeusizo yaliyomhusu Mtume Muhammad (S.A.W). Anashikwa na hasira. Mfalme Jeusizo anasimulia kana kwamba aliwafahamu Mtume Muhammad (S.A.W) na Ali vyema. Anasema kuwa kulikuwa na uadui kati ya Wakristo na Waislamu uliokuwa kama ule wa pamba na moto. Sifa za Khalid, Mikdad na Ali zinabainishwa katika usimulizi wa Mfalme Jeusizo. Anasema kuwa Mtume Muhammad (S.A.W) ana simba watatu ambao ni Khalid, Mikdadi na Ali.

Wafuasi wa mtume pia wamepewa sifa nyingi kuhusu ukali wao. Mfalme Jeusizo anasimulia ni kana kwamba aliwafahamu na pia kufahamu ukali wao. Hizi sifa na kana kwamba aliona wakipigana au akawa mmoja wao ili kuzifahamu. Usimulizi uliotumika hapa ni wa nafsi ya tatu.

Msimulizi pia anasimulia kuhusu idadi ya watu waliokufa vitani ni kana kwamba alikuwa mahali pale kuthibitisha idadi hiyo. Anasema kuwa waumini waliokufa walikuwa mia saba na walipata kuingia peponi, nyoyo zao zikapata amani na malaika kuwasifu. Warumu walioagadunia walikuwa milioni moja nao waliingia motoni. Wafuasi waliwazika walioaga dunia kisha wakarejea tena vitani. Masimulizi haya yalishuhudiwa na kisha kusimuliwa.

Mtunzi anaelezea kumhusu Ali. Mtume Muhammad (S.A.W) alikuwa akisali huku akilia. Ali anaota kuwa mtume yuko vitani na hana wa kumsaidia. Anasema kuwa amevamiwa na hana wa kumwoko. Safari ya mwezi moja inamchukua masaa machache tu. Ni kana kwamba mtunzi amemwona Mtume Muhammad (S.A.W)

akiumia na Ali kuota na kutoka kuenda kumsaidia. Mtunzi ametumia usimulizi wa nafsi ya tatu kuwasilisha haya.

Usimulizi wa nafsi ya tatu pia unatumiwa na mtunzi kuelezea idadi ya watu walioenda vitani kumsaidia Mtume Muhammad (S.A.W). Ali alipofika watu wote walikuwa wameenda hakuna aliyebaki nyuma ila Fatuma tu. Fatuma alibaki kwa kuwa Mtume Muhammad (S.A.W) alimwambia asiende vitani. Usimulizi katika sehemu hii unamkuza na kumpatia Fatuma sifa ya utiifu. Watu wote wanapoenda vitani, yeye alikatazwa na aliweza kuitii amri hiyo ya Mtume Muhammad (S.A.W).

Kisa kuhusu namna ambavyo Ali alifika na kuanza vita kimesimuliwa kwa nafsi hii. Mtunzi anasema kuwa aliitumia Dhu L'Fikar (upanga). Anawauma watu kwa meno na kuwatazama tu mtu alikuwa anakufa. Katika sehemu hii mtunzi anamkuza mhusika Ali. Anaonyeshwa kuwa mwenye nguvu. Anawauwa watu wengi kwa muda mfupi tu. Pia ni jasiri kwa kuwa yuko tayari kupigana. Haelekei kuogopa idadi ya watu waliofika katika uwanja huo wa vita. Mhusika Ali amekuzwa kwa kiwango kikubwa.

Hadithi kuhusu Kidari imetolewa kwa mbinu ya kisimulizi. Mtunzi anasema kuwa Kidari alikuwa ni mtumwa na Katirifu alimtegemea sana vitani. Alifahamu fika kuwa Kidari angemkinga kutokana na wapiganaji wengine. Katirifu anamtuma aende kumkamata Ali lakini hafaulu. Anakatwa masikio na kwa sababu ya aibu anajirusha motoni. Katika sehemu hii, mtunzi anamsifu Kidari kwa kuwa alikuwa hodari. Pili, anakusudia kuonyesha kuwa baadhi ya viongozi huwatumia watumwa kwa njia mbaya.

Matukio baada ya Katirifu kuuliwa yanasimuliwa kupitia kwa mbinu hii. Hasina anapopata habari kuwa Katirifu ameuliwa, anafika pale na kuvua nguo zote. Anamhukumu Katirifu na kusema kuwa mauti hayo alijitakia mwenyewe. Yalikuwa ni kwa sababu ya tamaa. Hata hivyo, mtunzi anaishia kumwonyesha Hasina kama mhusika aliyekuja kuamini kuwa Ali na Mtume Mohammad (S.A.W) walikuwa na nguvu kushinda binadamu yeyote yule.

Hatimaye mtunzi anatumia yaliyofanyika baada ya vita. Mali yote yaliyokusanywa yalipelekwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W) ili ayagawe kwa wale waliokuwepo. Mtume Muhammad (S.A.W) na wafuasi wake wanafunga safari kurejea Medina. Njiani anasoma aya na kumshukuru Mungu.

4.4 Hitimisho.

Matukio yote katika utenzi huu yamesimuliwa katika nafsi tofauti tofauti. Masimulizi haya hata hivyo yanaandikwa kwa muundo wa shairi. Katika sura hii, tumejadili matumizi ya usimulizi wa nafsi ya kwanza, pili na tatu huku tukitoa mifano kutoka kwenye *Utenzi wa Katirifu*.

SURA YA TANO.

HITIMISHO.

5.1 Muhtasari wa Yaliyoshughulikiwa Katika Utafiti Huu.

Katika sura hii tumetoa muhtasari wa tuliyoyashughulikia katika utafiti wetu ili kudhihirisha kuwa tulijikita katika malengo ya utafiti huu. Pili, tumeonyesha changamoto tulizokumbana nazo katika kuandika kazi hii na hatimaye, kuyatoa mapendekezo kwa watakaofanya tafiti za baadaye kuhusu *Utenzi wa Katirifu*.

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuonyesha namna ambavyo mtindo umetumika katika *Utenzi wa Katirifu*. Katika sura ya pili, tumehakiki wahusika na uhusika wao, sura ya tatu tukahakiki mbinu za lugha zilizotumiwa, sura ya nne mandhari na usimulizi ulivyotumika katika *Utenzi wa Katirifu* na hatimaye katika sura ya tano tumetoa muhtasari wa yote yaliyoshughulikiwa katika utafiti huu pamoja na mapendekezo kwa watafiti wa baadaye.

Kuwahusu wahusika, tumejadili mbinu mbalimbali zinazotumiwa katika usawiri wa wahusika wakawekwa katika makundi. Hatimaye, tulijadili sifa za wahusika na umuhimu wao katika utenzi wa *Katirifu*. Wahusika wengi wanadhihirika kuwa wa kihalisia kwa kuwa matendo yao yanalingana na mandhari ambamo wahusika wanaishi.

Tumezihakiki taswira, dayalojia na tamathali za usemikatika sura inayofuatia. Tumeshughulikia, maswali ya balagha, tashihisi, tashibihi, chuku na sitiari. Kwa kila tamathali tumejadili umuhimu wa matumizi ya tamathali hizo. Kwa kijumla, zimesaidia katika usawiri wa wahusika na pia kukuza na kuendeleza dhamira ya mwandishi wa kazi hii.

Hatimaye, tumeshughulikia mandhari na usimulizi katika sura ya nne. Kuna mandhari halisi na yasiyo halisi. Mandhari halisi yana maana ya yale yanayoweza kupatikana katika ulimwengu wa kawaida na yasiyo halisi ni yale yasiyoweza kupatikana katika mazingira ya kawaida. Ni ya kufikirika tu.

Kuna usimulizi wa nafsi ya kwanza, pili na tatu. Usimulizi hutegemea pakubwa lugha tumizi na sehemu (mandhari) ambamo matukio yanatokea. Usimulizi huwa na mchango mkubwa katika kazi yoyote ile ya fasihi. Kupitia usimulizi msikilizaji au msomaji hupata kuelewa yanayotendeka katika kazi fulani ya kifasihi. Vilevile kuna uhuru wa kishairi uliotumika kama vile inkisari, lahaja na matumizi ya maneno ya kale.

5.2 Changamoto.

Katika utafiti huu, tulipitia changamoto mbalimbali zikiwemo kutopata muda **wa** kutosha wakati tulipokuwa uwanjani tukifanya utafiti. Pili, ni tatizo la kifedha kwa kuwa kazi hii ilihitaji kuchapishwa baada ya marekebisho ya mara kwa mara ili kazi hii ionekane kuwa nzuri.

Tatu, tulikumbana na matatizo ya uhaba wa makala yaliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili. Kazi nyingi zilihita tafsiri hivyo baadhi ya tafsiri kukosa kuwepo na ulinganifu wa maana.

5.3 Mapendekezo kwa Tafiti Za Baadaye.

Tumeuchagua na kuufanyia uhakiki *Utenzi wa Katirifu* huu kama mwongozo tu kwa watafiti wa baadaye. Huu ni utenzi mmoja tu kati ya tenzi nyingine nyingi za Kiswahili zinazoweza kufanyiwa uhakiki wa kimtindo kama huu tulioufanya.

Katika *Utenzi wa Katirifu*, ni sehemu ndogo tu iliyofanyiwa uhakiki ambayo ni mtindo. Mtindo huu umejumuisha wahusika na uhusika wao, tamathali za usemi,

mandhari na usimulizi. Tafiti za baadaye zinaweza kuchunguza maudhui katika *Utenzi wa Katirifu*.

Nadharia iliyotumika ni Umitindo. Tunapendekeza kuwa wahakiki wengine wanaweza kutumia nadharia nyingine tofauti kuhakiki kazi hii. Kwa mfano matumizi ya nadharia ya uhalisiajabu na udhanaishi zinaweza kusaidia katika kuhakiki utenzi huu.

Kipengele kingine ambacho kinaweza kufanyiwa uhakiki ni kile cha mwingiliano matini kati ya utenzi huu na tenzi nyingine. Mwingiliano huweza kuwa wa kihusika au hata mada kama vile *Utenzi wa Herekali*.

MAREJELEO.

- Abedi, K.A. (1954). *Sheria za kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Attenbernd, L. na Lewis, L. (1963). *Introduction to Literature Stories*. New York: Macmillan Company.
- Crystal, D. na Davy, D. (1969). "Investigating English Style." London: Longman.
- Hegel, G.W.F. (1979). *Introduction to Aesthetics*. Oxford: Oxford University Press.
- Kadenge, K. (1982). "Deviation and Foregrounding in Chosen Swahili Texts." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Kanyua, G. (2011). "Mtindo na namna unavyoendeleza maudhui katika Natala." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- King'eli, K. na Kemoli, A. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi. Acacia Stantex Limited.
- Kitsao, J. (1975). "A stylistic Approach Adopted for the study of Swahili Prose Texts." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Knappert, J. (1979). *Four Centuries of Swahili Verse: A library History and Anthology*. London: Heinmann Educational Books Ltd.
- Kuhenga, C. (1977). *Tamathali Za Usemi: Mtaala wa Kiswahili*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Leech, G. N. na Short, M. (1981). *Style in Fiction. A Linguistic Introduction to English Fictional Prose* 2nd Edition. Harlow: Longman Group Limited.
- Leech, G.N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group Ltd.
- Lugwiri, P.O. (2011). "Sitiari, Taashira na Tashbiha katika uwasilishaji wa dhamira katika Utenzi wa Tambuka." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Mbatia, H. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.
- Mlacha, S.A.K. (1991). "Point of View as a Stylistic Device in Kiswahili Novels." Juzuu la 58. Dar-es-Salaam. TUKI.
- Mohamed, S.A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili. Tamthilia, riwaya na Hadithi Fupi*. Nairobi: East African Educational Publishers Limited.
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*: Nairobi: East African Educational Publishers Limited.
- Mungai, P.K. (2005). "Uhakiki linganishi wa kifani wa tenzi za Mikidadi na Mayasa na Swifa ya Nguvumali." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

- Murumba, J. B. (2011). "Mtindo katika watu wa Gehena." Tasnifuya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Murungi, G. K. (2011). "Mtindo unavyoendeleza Maudhui katika Natala." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Muthoni, M. (2014). "Uhakiki wa Maudhui na Mtindo katika Tikitimaji." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Nzuki, P. (2003). "Fanikatika Mchezo wa Karata na Bara jingine." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Ouma, O.K. (2011). "Uhakiki wa maudhui teule katika Utenzi wa Nabii Isa." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Senkoro, F.E. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
- Swaleh, A. (1992). "Maudhui katika Utenzi wa Mwanakupona." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- TUKI (2006). *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili*. Toleo la Tatu. Dar es Salaam: TUKI.
- Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia Za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wales, K. (1990). *A Dictionary of Stylistics*. London: Pearson Education Ltd.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- (2003). *Kamusi ya fasihi. Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers Limited.
- (2008). *Kanzi ya Fasihi. Misingi na Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide- Muwa Publishers.